





KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, DODOMA-TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

# HOTUBA YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.), KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2026/2027




**APRILI 2026** **DODOMA**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2026/2027



**MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.),**
**Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



Mheshimiwa Deus Clement Sangu (Mb.)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu
(Kazi, Ajira na Mahusiano)



Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe (Mb.)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu
(TAMISEMI)



Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga (Mb.)
Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)



Mheshimiwa Rahma Riyadh Kisuo (Mb.)
Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu
(Kazi, Ajira na Mahusiano)



Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb.)
Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu
(TAMISEMI - Elimu)



Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif (Mb.)
Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu
(TAMISEMI - Afya)



Dkt. Jim James Yonazi
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Bunge, Uratibu na
Wenye Ulemavu)



Bi. Mary Ngelela Maganga
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu
(Kazi, Ajira na Mahusiano)



Bw. Adolf Hyasinth Ndunguru
Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)



Dkt. James Henry Kilabuko
Naibu Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)



Bi. Zuhura Yunus Abdallah
Naibu Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu
(Kazi, Ajira na Mahusiano)



Bw. Sospeter Mambile Mtwale
Naibu Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)



Mha. Rogatius Hussein Mativila
Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI – Miundombinu)



Bw. Atupele Webster Mwambene
Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu
(TAMISEMI - Elimu)



Prof. Tumaini Joseph Nagu
Naibu Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu
(TAMISEMI - Afya)

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2026/2027. Aidha, kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambazo zilichambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, sasa ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizopo chini yake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema iliyotuwezesha kukutana mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha na kupokea Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa

kipindi cha Mwaka 2025/2026 na mwelekeo wake kwa Mwaka 2026/2027. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Waislamu wote kwa kumaliza salama mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikukuu ya Eid el Fitri kwa amani na utulivu. Vilevile, niwatakie kila la heri Wakristo wote walio katika Mfungo wa Kwaresma na kuwatakia maandalizi mema ya Sikukuu ya Pasaka.

**SALAMU ZA POLE**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 25 Machi, 2026 tuliondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, mwanasiasa mahiri aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Isimani.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Waziri mahiri na mchapakazi katika Baraza la Mawaziri. Vilevile, nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika, waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, familia, ndugu, jamaa, marafiki, wafanyakazi, wananchi wa Jimbo la Isimani na Watanzania wote kwa ujumla kutokana na msiba huo.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa uhai wake Mheshimiwa Lukuvi alihudumu katika nafasi mbalimbali. Baadhi ya nafasi hizo ni Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba na Mkuu wa Mkoa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Vilevile, alikuwa Waziri katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na utendaji kazi, umahiri na uzoefu katika masuala ya siasa pamoja na ushawishi wake, mnamo tarehe 13 Juni, 2023 Mheshimiwa Rais alimteua kuwa Mshauri wake Siasa na Uhusiano wa Jamii. Vilevile, Mheshimiwa Lukuvi aliwahi kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa vipindi tofauti kati ya mwaka 2010 – 2015, 2021 – 2022 na mwaka 2024 hadi umauti ulipomfika.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Lukuvi pia alikuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani kwa kipindi cha miaka 31 hadi umauti ulipomfika. Mheshimiwa Lukuvi atakumbukwa kwa uongozi na uthubutu wake katika uratibu wa shughuli za Serikali pamoja na ushawishi mkubwa wa kisiasa katika nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa marehemu pumziko la amani. Amina!

8. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninatoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Halima Idd Nassor Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), kilichotokea tarehe 18 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam. Tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake na utumishi uliotukuka ndani ya Bunge lako Tukufu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 3 Februari, 2026 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe aliyekuwa Mbunge Mstaafu Viti Maalumu (Mkoa wa Tabora). Vilevile, aliwahi kuhudumu katika nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama Cha Mapinduzi ikiwemo Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania. Wakati wa uhai wake, aliwatumikia wananchi wa Tabora na Watanzania kwa ujumla kwa ari na uzalendo wa hali ya juu. Ninatoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa msiba huo.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, tarehe 19 Februari, 2026 tuliondokewa na Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Muadhama Polycarp Kardinali Pengo. Kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa ninatoa pole kwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, waumini wa Kanisa Katoliki pamoja

na ndugu jamaa na marafiki. Marehemu Kardinali Pengo atakumbukwa kwa mchango mkubwa alioutoa katika huduma za kiroho. Wakati wa uhai wake, alisisitiza watu wote waishi maisha ya uadilifu, upendo, umoja na mshikamano wa kitaifa. Tutaendelea kuenzi mchango wake katika kuwaletea maendeleo Watanzania katika nyanja zote.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 20 Machi, 2026 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliyekuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na kuweka rekodi ya kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama Kuu katika Afrika Mashariki na Kati. Pamoja na wadhifa huo, Mheshimiwa Julie Catherine Manning aliwahi kuhudumu nafasi ya Waziri wa Sheria. Nitumie nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Rais kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, wadau wote wa sheria pamoja na Watanzania wote. Mheshimiwa Julie Catherine Manning, atakumbukwa kwa alama kubwa aliyoiweka katika kuwainua wanawake na kuchagiza maendeleo ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 17 Februari 2026, nchi ilimpoteza Mwanamuziki Mkongwe Mzee Steven Hiza ambaye ni mtunzi na mwimbaji wa wimbo maarufu uitwao Tanzania yetu ndiyo

nchi ya furaha. Sina shaka mtakubaliana nami kuwa wimbo huo umekuwa ukichochea uzalendo na umoja wa Watanzania kwa miaka mingi tangu ulipotungwa kati ya mwaka 1966/1967. Ninatoa pole kwa wanafamilia, wapenzi wa muziki na Watanzania wote kwa ujumla. Mzee Hiza atakumbukwa kwa uzalendo wake alioudhihirisha kwa kutunga wimbo huo ambao ubora wake hata sasa haujachuja katika historia ya muziki.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha hivi karibuni, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa katika mikoa mbalimbali. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Lindi, Arusha, Manyara, Dodoma, Pwani, Ruvuma, Kigoma, Tanga, Dar es Saalam, Kilimanjaro na Singida. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na maafa yatokanayo na mafuriko, katika kipindi hiki wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na ajali mbalimbali. Nitumie nafasi hii kutoa salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa na ajali ya Boti iliyotokea tarehe 13 Machi, 2026. Ninatoa pole kwa waathirika wote wa ajali ya Boti ya Nungwi pamoja na wote waliopata ajali mbalimbali zikiwemo za gari na pikipiki. Ninawaombea

majeruhi wote uponyaji wa haraka na marehemu wote pumziko la amani. Amina!

## UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA MWAKA 2025/2026

15. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii adhimu kumpongeza sana Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na juhudi zake za kuwatumikia wananchi kwa mapenzi ya dhati. Sote ni mashahidi wa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo na kuonesha dira ya mwelekeo wa Taifa hususan katika kuitekeleza falsafa yake ya ***"Kazi na Utu - Tunasonga Mbele".*** Nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na wananchi wote kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa Rais wetu nguvu, ulinzi, afya njema na kila lililo la heri katika kuwatumikia Watanzania.

16. ***Mheshimiwa Spika***, sina shaka nyote mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026; na Malengo ya

Maendeleo Endelevu 2030. Kupitia usimamizi wa utekelezaji wa mipango hiyo, mafanikio makubwa yamepatikana kama yalivyoelezwa kupitia Bunge la 12, Mkutano wa 19, kikao cha pili na Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi uliofanyika Mei, 2025.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio hayo makubwa, wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo na kukuza ustawi wa wananchi. Baadhi ya ahadi zilizotolewa ni pamoja na zile zilizotekelezwa ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa na kuingia madarakani. Ahadi hizo, zililenga kuimarisha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji; kurasimisha sekta isiyo rasmi; na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya biashara ndogo na za kati na uendeshaji wa kampuni changa.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza katika Bunge la 13, Mkutano wa Pili, ahadi hizo zimetekelezwa kwa mafanikio makubwa kupitia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa pamoja na usimamizi madhubuti. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanza utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Kwanza kwa wananchi 1,457,602 sawa na kaya 276,004 zisizo na uwezo. Vilevile, kuanza kugharimia magonjwa

sugu ya Saratani, Figo, Moyo, Kisukari na Mifupa kwa watu wasio na uwezo; na kuondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipa gharama za matibabu na madeni.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa elimu, Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 29 Januari, 2026. Mpango huo wenye kaulimbiu ya ***'Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu Bila Shida'*** unalenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za ufundishaji.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni kuzinduliwa kwa Mpango wa Kitaifa wa Pamoja Kati ya Waajiri, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo Vikuu. Mpango huo uliozinduliwa tarehe 9 Februari, 2026 na Mheshimiwa *Balozi Dkt.* Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unalenga kujenga uwezo wa ubunifu na ujasiriamali kwa wanafunzi ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sekta ya maji, Serikali inaendelea kutekeleza miradi 10 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.58. Miradi hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Gridi ya Taifa ya Maji ya kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na mito mikubwa kwenda kwenye maeneo mbalimbali nchini.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine yaliyopatikana ni kutoa ajira na kuwapangia vituo vya kazi watumishi 12,000 ambapo kati ya hao, 5,000 ni wa sekta ya afya na 7,000 wa sekta ya elimu. Watumishi hao wameongeza ufanisi wa utoaji huduma katika sekta za afya na elimu.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri, tarehe 5 Februari, 2026 Serikali ilitoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kundi hilo. Fedha hizo zitaongeza uzalishaji wa ajira katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda na biashara, na mawasiliano na hivyo kuwezesha vijana kuongeza kipato na kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** hayo ni baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika siku 100 za utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita kipindi cha pili chini ya uongozi mahiri wa

Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wahenga walisema "**mwenye macho haambiwi tazama".** Mafanikio hayo ni ishara tosha ya misingi imara aliyoiweka Mheshimiwa Rais ya utekelezaji wa Dira 2050 katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza.

25. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa ahadi za siku 100 niliyoyaeleza, mafanikio mengine yaliyopatikana kisekta kwa mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

## HALI YA UCHUMI

### Ukuaji wa Uchumi

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2025, kiwango sawa na mwaka 2024. Mwenendo huo unatokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika teknolojia mpya, hususan teknolojia ya akili unde, pamoja na juhudi za nchi mbalimbali kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea shughuli za uzalishaji katika uchumi wao.

*27.* ***Mheshimiwa Spika,*** hapa nchini, uchumi umeendelea kukua kwa kasi ambapo katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2025, pato halisi la Taifa limekua kwa asilimia 6.0

ikilinganishwa na asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na uwekezaji mkubwa katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ikiwemo nishati, mawasiliano, usafiri na usafirishaji, huduma za kijamii na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika ngazi ya kikanda, uchumi wa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara umeendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na kuimarika kwa uwekezaji katika miundombinu, kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji na kuimarika kwa mauzo ya bidhaa katika soko la kimataifa. Uchumi wa ukanda huo unatarajiwa kuendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2026 na 2027. Aidha, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2025 na 2026, hali inayoonesha uwezo mkubwa wa ukanda huo kuwa moja ya maeneo yenye ukuaji wa kasi zaidi barani Afrika.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kubaki katika wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2026 na kushuka hadi asilimia 3.2 mwaka 2027. Hali hiyo itawezesha uchumi wa dunia kuendelea kuwa himilivu

licha ya changamoto zinazotokana na migogoro ya kikanda, mabadiliko ya sera za biashara na hali ya kifedha ya kimataifa.

**Mfumuko wa Bei**

30. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kuwa na utulivu wa bei uliotokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha, kuimarika kwa bei ya mafuta na bidhaa katika soko la dunia na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani. Utulivu huo ulichangia kupunguza kasi ya ongezeko la bei ya bidhaa na huduma. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.5. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 3.0 hadi 5.0.

31. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mfumuko wa bei kwa Januari, 2026 ulikuwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutozidi asilimia 8.0 na lengo la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la asilimia 3.0 hadi 7.0. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia hali ya kisiasa na kiuchumi duniani na kuchukua hatua stahiki ili kuwa na utulivu wa mwenendo wa bei za bidhaa.

## Mauzo ya Nje na Akiba ya Fedha za Kigeni

32. ***Mheshimiwa Spika,*** mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 16.3 Januari, 2025 hadi dola za Marekani bilioni 18.7 Januari, 2026 sawa na ongezeko la asilimia 12.7. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya bidhaa mbalimbali ikiwemo dhahabu, tumbaku, kahawa, bidhaa za viwandani, utalii na huduma za usafirishaji. Aidha, Januari, 2026, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 6.3. Kiasi hicho, kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa zaidi ya miezi 4.8 ikiwa ni juu ya kiwango cha chini kinachokubalika kimataifa.

## Mikopo kwa Sekta Binafsi

33. ***Mheshimiwa Spika,*** mikopo iliyotolewa na benki kwa sekta binafsi imeongezeka kutoka asilimia 12.8 Januari, 2025 hadi asilimia 23.5 Januari, 2026. Mikopo hiyo, imenufaisha na kuchochea shughuli za uwekezaji pamoja na uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo madini, biashara, kilimo, viwanda, usafirishaji na ujenzi.

**Mwenendo wa Mapato**

34. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato. Kutokana na jitihada hizo, shilingi trilioni 26.63 zilikusanywa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari, 2026 kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 25.68, sawa na ufanisi wa asilimia 103.7 na ukuaji wa asilimia 19.27 ikilinganishwa na mapato ya shilingi trilioni 22.32 yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025.

35. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya mapato hayo, shilingi trilioni 22.09 ni mapato yaliyotokana na kodi, shilingi trilioni 3.78 ni mapato yasiyo ya kodi na shilingi bilioni 754.26 ni misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kati ya fedha zilizokusanywa, shilingi trilioni 12.28 zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo mradi wa SGR; Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato; ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya na elimu; miradi ya maji; miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji; na skimu za umwagiliaji.

36. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli ya mikoa na mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, hadi Februari, 2026 shilingi trilioni 1.08 zimekusanywa kati ya lengo la shilingi trilioni 1.68 sawa na asilimia 64.61 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 172.87 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.08 ni mapato ya ndani ya halmashauri. Makusanyo hayo yalitokana na tozo, madeni na mauzo ya bidhaa mbalimbali.

37. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kusimamia ukusanyaji wa kodi za majengo. Hadi Februari, 2026 shilingi bilioni 61.13 zimekusanywa kutoka kwenye kodi ya majengo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 48.9 zimewasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na shilingi bilioni 12.23 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya majengo.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha mfumo wa kodi nchini na kuufanya kuwa jumuishi, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliunda Tume ya Kutathmini Maboresho ya Mfumo wa Kodi nchini. Lengo lilikuwa ni kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa kodi kufuatia malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafanyabiashara,

wawekezaji pamoja na wadau wa maendeleo ili kuandaa mapendekezo ya kuboresha mfumo huo.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilikamilisha kazi hiyo na kuwasilishwa taarifa kwa Mheshimiwa Rais tarehe 18 Machi, 2026. Taarifa hiyo imeainisha kuwa, maboresho ya mfumo wa kodi ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya muda mrefu yaliyoainishwa katika Dira 2050. Vilevile, imeainisha mikakati mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kodi.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** niendelee kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa moyo wa uzalendo na maamuzi sahihi ya kufanya mapitio makubwa ya mfumo mzima wa kodi nchini ambayo hayakufanyika kwa kipindi cha miaka 30. Utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa hiyo utawezesha kuongeza wigo wa kodi na kuhakikisha kila mtu anachangia kadri ya kipato chake.

41. ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia mikakati itakayoongeza ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini;

kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA. Mikakati hiyo itahakikisha shabaha za uchumi jumla zilizobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 zinafikiwa.

**Dira 2050**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imekuwa ikiongozwa kwa mipango thabiti ya maendeleo. Sote tunakumbuka kuwa katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, tuliongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ilitafsiriwa katika mipango mitatu ya maendeleo ya Taifa ya miaka mitano. Mpango wa kwanza Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2011/2012 - 2015/2016 ukiwa na dhima ya "Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi".

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 ukiwa na dhima ya "Kukuza Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu". Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulitekelezwa mwaka 2021/2022 – 2025/2026, ukiwa na dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu" ambao ndiyo unakamilisha utekelezaji wa Dira 2025.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 17 Julai, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo itaongoza mipango yetu ya maendeleo katika miaka 25 ijayo. Vilevile, inalenga kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi kwa wote, lenye haki na linalojitegemea. Kama sehemu ya mkakati wa utekelezaji wa Dira 2050, Serikali iliandaa na Bunge lako likapitisha katika mkutano uliopita Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utakaotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano 2026/2027 – 2030/2031. Dhima ya mpango huo ni "Mageuzi katika Kukuza Uchumi na Kuzalisha Ajira".

45. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti itakayopitishwa na Bunge hili ni hatua ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 - 2030/2031 na Dira 2050. Utekelezaji wa Dira hiyo, utawezesha Taifa kuwa na uchumi wenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja na wastani wa pato la mtu mmoja mmoja kuwa dola za Marekani 7,000 kwa mwaka ifikapo 2050.

46. ***Mheshimiwa Spika***, Dira 2050 ndiyo mwelekeo wa Taifa letu. Kwa kuzingatia hilo kipaumbele cha Serikali kitawekwa katika

utekelezaji wa malengo kama yalivyobainishwa katika Dira hiyo. Suala hilo litawezekana ikiwa wadau wote watakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira 2050. Nitoe rai kwa viongozi wa Serikali, Dini, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Wadau wa Maendeleo kuhakikisha kwamba mipango yao inawiana na vipaumbele vya Dira 2050 na kuiunga mkono katika utekelezaji wake. Aidha, ninailekeza Tume ya Mipango kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Dira 2050 ili kuwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji.

## UWEKEZAJI NA UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kujenga uchumi unaoongozwa na uwekezaji kutoka sekta binafsi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Ili kuonesha dhamira ya dhati ya kutekeleza malengo hayo, katika mwaka 2025/2026, miradi 927 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 11.08 ilisajiliwa. Hatua hiyo, inaonesha kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini na kuongezeka kwa imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uwekezaji huo, Serikali imeendeleza maeneo maalum ya uwekezaji ili kuimarisha ukuaji wa uchumi wa viwanda na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutenga Maeneo Maalum ya Kiuchumi 34 na kuendelea na utekelezaji wa miradi 25 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 280.8. Miradi hiyo inatarajiwa kuzalisha mauzo ya nje yenye thamani ya dola za Marekani milioni 672.63. Mikakati mingine ni pamoja na kupunguza tozo 245; kurekebisha sheria 28; na kuimarisha utoaji wa huduma kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania. Jitihada hizo zimeendelea kuboresha mazingira ya biashara na kupunguza gharama za uwekezaji.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uwekezaji unaofanyika unakuwa na manufaa kwa Watanzania na kuzingatia mipango ya ndani ya nchi, Serikali imeimarisha ulinganifu wa sera, mipango na bajeti ili taasisi zote zitekeleze vipaumbele vya Taifa kwa mwelekeo mmoja. Vilevile, imeweka kipaumbele katika usimamizi wa miradi ya kielelezo ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati, kwa gharama zilizopangwa na viwango vinavyotarajiwa. Hatua hiyo inalenga kuharakisha matokeo katika kukuza uchumi, kuongeza ajira, kuimarisha uzalishaji viwandani na kuboresha huduma kwa wananchi.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua zinazochukuliwa zinaakisi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga uchumi wa matokeo unaoongeza tija katika sekta za uzalishaji. Licha ya hayo, hatua hizo zinaongeza kipato cha Mtanzania mmoja mmoja na hivyo kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu wenye pato la taifa la takribani dola za marekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendeleza uwekezaji wa kimkakati katika maeneo mbalimbali ikiwemo Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo, Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa Magadi Soda Engaruka. Vilevile, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kukuza na kuvutia uwekezaji nchini na kuratibu utekelezaji wa Dira 2050 kupitia mipango ya mwaka na muda wa kati.

## SEKTA ZA UZALISHAJI

### Kilimo

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Baba wa Taifa na mwanafalsafa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake kiitwacho *Mtu na Maendeleo (1974)* alisema kuwa, ninaomba kunukuu **"maendeleo ya kweli huanza pale wananchi wanapoweza kuzalisha chakula cha kuwatosha wenyewe**" mwisho wa kunukuu.

Serikali kwa kutambua umuhimu huo, imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa chakula ambapo tani 23,783,128 zilizalishwa katika msimu wa mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 18,279,054 kwa mwaka 2025/2026 na hivyo kuihakikishia nchi usalama wa chakula kwa asilimia 130.

53. ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko la uzalishaji limetokana na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati na Serikali kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea. Aidha, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026, Serikali imetoa tani 1,098,990 za mbolea sawa na asilimia 73.26 ya lengo. Kati ya hizo, tani 574,664.99 zenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.03 zimesambazwa kwa wakulima 526,044 kupitia mpango wa ruzuku. Hatua hiyo ilichochea ongezeko la matumizi ya mbolea na tija katika uzalishaji.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** upatikanaji wa uhakika wa mbolea umeongeza matumizi ya mbolea kwa asilimia 14.6 kutoka tani 848,884 mwaka 2023/2024 hadi tani 972,506 mwaka 2024/2025. Vilevile, matumizi ya virutubisho yameongezeka kutoka kilogramu 19 hadi 24 kwa hekta na hivyo kuonesha mwitikio chanya wa wakulima na mafanikio ya mikakati ya Serikali ya kuhamasisha kilimo chenye tija.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na upatikanaji wa mbolea, Serikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Januari 2026, jumla ya tani 61,003.42 za mbegu zimepatikana. Kati ya hizo, asilimia 58.31 zimetokana na uzalishaji wa ndani ya nchi. Aidha, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi na kuzalisha miche zaidi ya milioni 28 ya mazao mbalimbali kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima. Hatua hiyo inalenga kuongeza uzalishaji na kupunguza utegemezi wa mbegu kutoka nje ya nchi.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha kilimo cha kisasa na kuwainua wakulima wadogo, Serikali imeanzisha vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo. Vilevile, imenunua matrekta 360 na kuyaweka kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakulima.

57. ***Mheshimiwa Spika***, ili kurasimisha na kuimarisha huduma za ugani kwa kuwafikia wakulima kwa wakati bila kupitia mlolongo mrefu, Serikali ipo kwenye hatua za kuanzisha Wakala ya Huduma za Ugani Kilimo. Lengo ni kuongeza tija kwa wakulima kwa kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi ya kilimo, kuhaulisha teknolojia, kutoa ushauri wa kilimo bora na matumizi ya mbinu endelevu.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, Serikali imeendelea kutekeleza miradi 146 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Kati ya hiyo, ujenzi wa skimu 20 na mabwawa 6 ya umwagiliaji umekamilika. Juhudi hizo zimeongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 727,280.06 mwaka 2024/2025 hadi hekta 983,466.60 mwaka 2025/2026.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miundombinu ya masoko, Serikali imeimarisha masoko ya mazao kwa kuendelea na ujenzi wa masoko matano ya kimkakati katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama (Busoka) na Halmashauri za Wilaya za Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Ujenzi wa masoko hayo umefikia wastani wa asilimia 81.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ujenzi wa vituo sita vya masoko katika Halmashauri ya Mji wa Nzega (Ushirika) na Halmashauri za Wilaya za Karatu (Endashangwet), Mpwapwa (Kibakwe), Monduli (Losirwa), Rombo (Mamsera) na Hai (Masama mula) umefikia wastani wa asilimia 29.3. Kukamilika kwa ujenzi wa masoko na vituo hivyo kutarahisisha ukusanyaji na uuzaji wa mazao ndani na nje ya nchi na kuongeza kipato cha mkulima.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta tija inayotarajiwa katika kilimo, naelekeza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mpango mahsusi wa usimamizi wa katazo la utaratibu wa lumbesa. Aidha, mazao yote yanayofungashwa kwenye vifungashio yauzwe kwa kuzingatia vipimo. Suala hili litekelezwe sambamba na udhibiti wa ushuru holela wa mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na Halmashauri zote kusitisha mara moja ushuru holela unaotozwa kwa mazao ya kilimo. Vilevile, kusitisha utaratibu wa wakulima kukopwa mazao na AMCOS.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, afya ya udongo, hifadhi ya chakula na masoko ya mazao. Lengo kuu ni kuongeza uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kukuza kilimo biashara na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi.

**Mifugo**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya mifugo kwa kuboresha mazingira ya ufugaji na biashara ya mifugo. Jitihada zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa karantini ya Kwala Mkoani Pwani yenye thamani ya

shilingi milioni 997.99 ambapo umefikia asilimia 45. Kukamilika kwa karantini hiyo itawezesha kuongeza idadi ya mifugo itakayokidhi vigezo vya kusafirishwa nje ya nchi.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa minada 21 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.76 katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Mara, Mwanza, Dodoma, Geita, Singida, Iringa, Tabora, Simiyu, Tanga, Shinyanga, Kagera na Arusha. Pia, Serikali imekamilisha ujenzi wa mabwawa mawili na inaendelea na ujenzi wa mabwawa 6 yaliyo katika hatua mbalimbali. Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa hayo utakaogharimu shilingi bilioni 5.44 utawezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika kipindi chote cha mwaka.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendesha kampeni ya kitaifa ya chanjo ambapo mifugo milioni 49.4 kati ya milioni 76.3 sawa na asilimia 64 imechanjwa. Sambamba na hilo, imeendelea na zoezi la utambuzi wa mifugo na kusambaza vifaa vya chanjo.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utoaji wa chanjo, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu za malisho kwa kuzalisha tani 149.9 zilizosambazwa kwa wafugaji katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Upatikanaji wa malisho ya uhakika ni muhimu katika kufikia lengo la ufugaji endelevu na

kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

**Uvuvi**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko katika Mkoa wa Lindi kwa gharama ya shilingi bilioni 280.58 ambazo ni fedha za ndani. Hadi Februari 2026, ujenzi umefikia asilimia 95. Kukamilika kwa bandari hiyo kutaimarisha utoaji wa huduma kwa wavuvi wakubwa na wadogo wa ndani na nje ya nchi, kuzalisha ajira 30,000 na kuboresha miundombinu ya uvuvi ili kupunguza kiwango cha umaskini.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa uvuvi katika Bahari Kuu, Serikali imenunua meli maalumu ya uvuvi kwa njia ya mishipi yenye urefu wa mita 22 iliyowasili nchini Februari, 2026. Meli hiyo itawezesha uvuvi wa Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) na hivyo kuongeza kiwango cha uvuvi, kukuza ajira na ujuzi hasa kwa vijana na kuongeza pato la wananchi na Taifa kwa ujumla.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imetoa mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji kwa ajili ya kuwawezesha kuendeleza shughuli za uvuvi ikiwemo ununuzi wa boti 219 na boti saidizi 118. Kadhalika, imetoa elimu kwa wadau zaidi ya 254,000 katika mnyororo wa thamani wa uvuvi na kuzalisha vifaranga vya samaki vilivyosambazwa katika maeneo mbalimbali.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango na umuhimu wa shughuli zinazotekelezwa na wavuvi wadogo, kamati za usalama ziimarishe ulinzi katika maeneo yote ambapo shughuli za uvuvi zinafanyika. Aidha, ni lazima kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na utu wakati wa kuwasimamia wavuvi wadogo kwenye shughuli zao za kila siku.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kufanya tafiti za kimkakati katika uzalishaji wa mnyororo wa thamani wa uvuvi, kutekeleza mikakati ya uvuvi katika bahari kuu ikiwemo ununuzi wa meli na ujenzi wa bandari ya uvuvi. Vilevile, kudhibiti magonjwa ya mifugo kupitia ununuzi wa chanjo, ujenzi wa majosho na kuendeleza miradi ya kuongeza tija, ajira na mapato ya Taifa.

## Maliasili na Utalii

*72.* ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maliasili na Utalii imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, ajira na pato la Taifa. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuinua sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Mikakati hiyo imeongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi za Taifa kwa asilimia 10.73 kutoka watalii 5,360,247 mwaka 2024 hadi 5,935,561 mwaka 2025 na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 hadi dola za Marekani bilioni 4.4 Desemba 2025 sawa na ongezeko la asimilia 12.82.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la watalii limechangiwa kwa kiasi kikubwa na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zimetambuliwa kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kutambua mchango huo, tarehe 31 Januari, 2026, Mheshimiwa Rais alitunukiwa tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono katika hafla ya utoaji tuzo ya *Serengeti Awards*.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** isitoshe, Tanzania imechaguliwa kuwa mwanachama wa Kamati ya Urithi wa Dunia na kushinda tuzo mbalimbali zilizotolewa na taasisi ya *World Travel Awards*. Tuzo hizo ni Tanzania kuwa Kituo Bora Duniani kwa Utalii wa Safari; Serengeti kuwa Hifadhi Bora Duniani; Zanzibar kuwa Kituo Bora cha Mikutano ya Kampuni na Mapumziko; Kampuni ya *Serengeti Balloon Safaris* kushinda nafasi ya Kampuni Bora ya Safari za Puto Duniani; na Kisiwa cha Jumeirah Thanda kilichopo Mafia kushinda nafasi ya Kisiwa Bora cha Mapumziko Duniani.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa, Serikali ilipokea ripoti ya Tume ya Rais ya Kutathmini Zoezi la Uhamaji wa Hiari wa Wakazi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Tume ya Rais ya Kutathmini Masuala ya Ardhi katika Wilaya ya Ngorongoro. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa Serikali itafanyia kazi mapendekezo ya ripoti hizo kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu na kuimarisha utalii katika ukanda huo.

**Madini**

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya madini kwa kutekeleza mikakati mbalimbali inayoongeza mapato ya Serikali na fursa za ajira kwa wananchi. Kama

ilivyo sekta ya Maliasili na Utalii, sekta ya madini ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, mikakati mbalimbali imeendelea kutekelezwa ikiwemo kuimarisha usimamizi na utendaji wa masoko 44 na vituo 118 vya ununuzi wa madini.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza rasilimali muhimu ya madini, Serikali imesaini makubaliano ya kuendeleza Mradi wa Niobium wa Panda Hill, Mkoani Mbeya ambao utakuwa kitovu cha uzalishaji na usindikaji wa madini mkakati. Kupitia mradi huo, Tanzania inalenga kuwa mzalishaji wa nne duniani kwa kuchangia takriban asilimia 4 ya mahitaji ya dunia na kuzalisha takriban tani 100,000 kwa mwaka.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi huo utakaokuwa na uwekezaji wa awali wa dola za Marekani milioni 442, Serikali inatarajia kupata mapato ya takribani shilingi trilioni 2 kutokana na mrabaha, kodi pamoja na gawio la hisa za Serikali ambazo zitachangia katika maendeleo ya miundombinu na huduma muhimu za kijamii kama barabara, shule na hospitali. Aidha, zaidi ya watu 1,600 wanatarajiwa kuajiriwa.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Serikali inatambua nafasi ya wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini katika kuendeleza sekta hiyo muhimu. Hivyo, imetoa leseni 8,418 za uchimbaji madini. Kati ya leseni hizo, za uchimbaji mdogo ni 5,983, leseni ndogo za biashara ni 1,339, leseni za uchimbaji wa kati ni 14, leseni za utafutaji ni 207, leseni kubwa za biashara ni 848 na leseni za uchenjuaji ni 27.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imewawezesha wachimbaji wadogo 1,239 kwa kuwapatia mafunzo kuhusu uchimbaji salama, utunzaji wa mazingira, huduma ya uchorongaji, uchenjuaji na afya migodini sambamba na kuwatengea maeneo 99 ya uchimbaji madini. Mikakati hiyo imewezesha kukusanya mapato ya madini ya shilingi bilioni 771.53 sawa na asilimia 64.3 ya lengo la shilingi trilioni 1.2 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Januari, 2026 na hivyo kuchangia uendeshaji wa miradi ya maendeleo.

81. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha Taifa kuwa na taarifa za uhakika kuhusu kiasi na ubora wa rasilimali za madini, ninaelekeza Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Madini kuweka utaratibu wa kutenga fedha zitokanazo na mapato ya madini kwa ajili ya tafiti za utafutaji wa madini. Utaratibu huo uanze kutumika mwaka 2026/2027.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ili kutoa fursa kwa Watanzania kunufaika na rasilimali za madini, ninaelekeza Wizara ya Madini kuweka utaratibu wa kudhibiti mikataba wanayoingia Watanzania wenye vitalu na wawekezaji wa nje ili kulinda maslahi ya Watanzania na Taifa. Hatua hii itasaidia pia kuondoa migogoro kati ya wachimbaji wadogo na wawekezaji wakubwa.

83. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati. Vilevile, itahamasisha uwekezaji, kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito, kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za madini za kina na kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

## Nishati

### *Umeme*

84. ***Mheshimiwa Spika***, sina shaka, nyote mtakubaliana nami kwamba, nishati ya umeme ni injini ya kuharakisha na kurahisisha maendeleo ya kisasa hususan inapotumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanda, teknolojia pamoja na matumizi ya nyumbani. Serikali kwa kutambua hilo, imeendelea

kutekeleza mikakati mahsusi ya kuhakikisha nishati ya umeme inayozalishwa hapa nchini, inakidhi mahitaji yatokanayo na kasi kubwa ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka kilomita 7,745.4 mwaka 2025 hadi kufikia kilomita 8,500.38 Februari, 2026. Pia, imekamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa MW 50 kwa kutumia jua katika Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga.

86. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Chalinze kupitia Kinyerezi hadi Mkuranga (kilomita 135) ambao umefikia asilimia 53.53, na kutoka Chalinze hadi Dodoma (kilomita 345) ambao umefikia asilimia 64.14. Kukamilika kwa miradi hiyo kutawezesha umeme unaozalishwa katika Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere kusambazwa katika Mikoa mbalimbali na hivyo kuendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuchochea kasi ya ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya Kitongoji, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuhakikisha nishati ya

umeme inafika katika maeneo hayo. Hadi Februari, 2026, jumla ya vitongoji 39,003 kati ya 64,359 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 61 vimeunganishwa na huduma ya umeme. Aidha, kazi ya kupeleka umeme katika vitongoji 9,009 vya Tanzania Bara kupitia mradi wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2 inaendelea.

88. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kukamilika kwa miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ikiwemo ujenzi wa bwawa la Julius Nyerere kwa kutumia fedha za ndani, hivi sasa nchi ina ziada ya umeme. Aidha, Serikali itaendelea kujenga na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa umeme ili kuondoa changamoto ya kukatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuunganisha wilaya ambazo hazipo katika gridi ya Taifa.

89. ***Mheshimiwa Spika***, ninaelekeza Wizara ya Nishati ikamilishe utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme katika vitongoji. Vilevile, iweke kipaumbele katika kuunganisha umeme katika hospitali, vituo vya afya, zahanati, shule, taasisi za dini na visima vya maji. Aidha, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kuimarisha utekelezaji wa wa mradi wa Gridi Imara ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatolewa kwa wakati. Lengo ni kuondoa tatizo la kukatika mara kwa mara kwa umeme nchini.

***Mafuta na Gesi***

90. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na juhudi za upatikanaji wa nishati ya umeme, Serikali imeendelea kuhakikisha ongezeko la matumizi ya gesi asilia. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari, 2026, Serikali imeongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika viwanda, taasisi na nyumbani hadi kilomita 243.6 ikilinganishwa na kilomita 184.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa vituo 14 vya kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa ili kutoa huduma ya usambazaji wa gesi asilia kwenye vyombo vya moto.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa, ninaelekeza Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Nishati zishirikiane kuandaa viwango msawazo *(specifications)* vitakavyoainisha mahitaji ya vyombo vya moto vya Serikali. Vilevile, zijenge miundombinu ya kutosha kuwezesha vyombo hivyo kuanza kutumia gesi asilia iliyoshindiliwa.

92. ***Mheshimiwa Spika***, licha ya uwepo wa changamoto za kiusalama kikanda na kimataifa ikiwemo ile ya Mashariki ya Kati, Serikali imeendelea kusimamia upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli na kuhakikisha bei ya bidhaa hizo inaendelea kuwa himilivu. Usimamizi

huo umewezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kutekelezwa bila kuathiriwa na changamoto yoyote.

93. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kusimamia mifumo ya kuagiza, kuhifadhi na kusambaza mafuta pamoja na kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Mtwara. Katika kufanikisha hilo, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa ghala la kupokea na kuhifadhi mafuta lenye uwezo wa kupokea tani 308,110 katika Bandari ya Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 30. Aidha, miundombinu ya kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Mtwara imeongezeka kutoka tani 29,280 hadi tani 110,221 ambayo itawezesha kupokea meli yenye shehena ya tani 30,000.

94. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani – Tanga umefikia asilimia 81 ikilinganishwa na asilimia 52 zilizokuwa zimefikiwa Februari, 2025. Hii ni hatua kubwa na mradi unatekelezwa kwa viwango tarajiwa. Kama nilivyoelekeza nilipotembelea mradi huo hivi karibuni, mradi utakapokamilika, kipaumbele cha kutoa ajira kiwe kwa wale waliofanya kazi wakati wa ujenzi wa mradi. Lengo ni kuendeleza utaalamu uliopatikana

kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine inayotekelezwa na Serikali na wadau.

95. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia ili kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanaacha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo mwaka 2034. Jitihada zilizochukuliwa na Serikali hadi Februari, 2026 ni pamoja na kugawa majiko banifu 13,575 kwa ruzuku ya asilimia 85, mitungi ya gesi asilia 28,653 ya kilo sita kwa ruzuku ya asilimia 50 na majiko janja ya umeme 7,292. Vilevile, Serikali imewezesha taasisi 1,136 zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hatua hizo zitasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira na kulinda afya za wananchi wanaotumia nishati hiyo.

96. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kukidhi mahitaji ya nishati nchini; kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havijapatiwa umeme; kuendeleza shughuli za kutafuta, kusafirisha, kuhifadhi na kusambaza mafuta na gesi asilia. Pia, kukamilisha mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi na kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa

Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034).

**Ardhi**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya ardhi ni muhimu katika kuwezesha uzalishaji na maendeleo ya sekta nyingine. Hata hivyo, sekta hiyo imekumbwa na changamoto na migogoro mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo mengi kutopimwa, ucheleweshaji wa utoaji wa hati, umilikishaji wa eneo moja kwa zaidi ya mtu mmoja na baadhi ya watendaji kutokuwa waaminifu. Changamoto hizo zimesababisha uwepo wa migogoro baina ya makundi mbalimbali katika jamii yakiwemo ya wakulima na wafugaji. Pia migogoro ya mipaka baina ya vijiji.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutatua migogoro iliyopo kupitia kliniki za ardhi, kamati za wataalamu, mabaraza ya ardhi na ziara za viongozi. Hadi Januari, 2026 migogoro 5,333 imetatuliwa, maombi ya umiliki 10,113 yalipokelewa na hatimiliki 7,182 ziliandaliwa pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 191.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninaelekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufanya tathmini kwa lengo la kuboresha mifumo ya kushughulikia migogoro ya ardhi. Vilevile,

kuendelea kutatua changamoto zilizopo kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo kuimarisha matumizi ya TEHAMA.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha changamoto na migogoro hiyo inafikia kikomo, ninaelekeza Wizara ya Ardhi kuhakikisha watumishi wake wote wanapimwa utendaji kazi wao kwa idadi ya changamoto na migogoro waliyoitatua pamoja na hati walizotoa. Vilevile, hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi wote watakaobainika kuwa chanzo cha migogoro hiyo. Aidha, Wizara ihakikishe taratibu na mifumo inayotumika katika kutoa huduma za ardhi, inakuwa ya wazi na rafiki kwa wananchi wote.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia upangaji na upimaji wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; na kuboresha huduma za uthamini na ulipaji fidia. Vilevile, itaimarisha utatuzi wa migogoro, kuendeleza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani ili kuongeza tija, uwazi na kasi ya utoaji huduma.

## Viwanda na Biashara

102. ***Mheshimiwa Spika***, sekta ya viwanda na biashara inaendelea kuwa nguzo muhimu katika kuleta mageuzi ya kiuchumi nchini. Hii ni kutokana naukweli kwamba, sekta hiyo ni kichocheo katika ukuaji wa Pato la Taifa, kuongeza ajira, kuvutia uwekezaji na kuimarisha ushindani wa Tanzania katika masoko ya kikanda na kimataifa.

103. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuwezesha ujenzi wa kongani ya *Sino Tan Industrial Park* (Kwala) ambao umefikia asilimia 80 na viwanda 4 vimeanza uzalishaji. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa miundombinu muhimu katika kongani ya *Modern Industrial Park* (Mlandizi) na ujenzi wa viwanda 5 unaendelea. Kukamilika kwa kongani hizo kutachangia kuzalisha ajira zaidi ya 130,000.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** uwepo wa viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa mbalimbali ni hatua muhimu ya kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. Moja ya bidhaa ambayo imekuwa ikiagizwa kutoka nchi za nje kwa fedha za kigeni ni sukari ya viwandani. Hata hivyo, kuanzia Novemba, 2025 Kiwanda cha Sukari Mkulazi kilianza rasmi uzalishaji wa sukari ya viwandani ambapo hadi Februari,

2026 tani 256 zilizalishwa. Uzalishaji huo unatarajiwa kupunguza mahitaji ya uagizaji wa sukari ya viwandani kutoka nje kwa asilimia 20 kwa mwaka. Kiwanda hicho ni cha kwanza kuzalisha sukari ya viwandani ndani ya nchi.

105. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya viwanda nchini ambapo katika mikoa tisa, tathmini imekamilika na kuwezesha kutambuliwa kwa viwanda 25,650 vilivyoingizwa kwenye kanzidata. Tathmini hiyo itawezesha Serikali kupanga mipango ya kuviendeleza kwa kuzingatia mahitaji ya msingi ili kuongeza mchango wa viwanda hivyo katika kuzalisha ajira na kuchangia kukua kwa uchumi.

*106.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa biashara, Serikali imekamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Mkakati huo utawezesha Tanzania kufikia soko la zaidi ya watu bilioni 1.4 lenye thamani ya zaidi ya dola za Marekani trilioni 3.4. Vilevile, imesaini mkataba wa Mfumo Rahisi wa Biashara na Malawi kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo.

107. ***Mheshimiwa Spika***, mkataba huo unalenga kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wa mpakani kununua na kuuza kwa urahisi kupitia mifumo iliyorahishwa ya

nyaraka za kiforodha na vyeti vya uasili wa bidhaa ukihusisha bidhaa 61. Vilevile, wafanyabiashara hawatalipa ushuru wa forodha kwa bidhaa zilizo ndani ya kiwango cha dola za Marekani 2,000 kwa siku. Aidha, utekelezaji wa mkataba huo utasaidia kuhamasisha wafanyabiashara wadogo kurasimisha biashara zao na kutumia njia rasmi za ufanyaji biashara na hivyo kuongeza biashara baina ya Tanzania na Malawi.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hayo, Serikali imesaini tamko la kuanzisha Kamati ya Pamoja ya Biashara kati ya Tanzania na Uturuki, hatua itakayosaidia kuongeza ujazo wa biashara. Vilevile, imeanza utekelezaji wa Mkataba wa Eneo la Biashara Huru la Utatu ambalo ni COMESA, EAC na SADC unaopanua fursa za biashara kwa wafanyabiashara wa Kitanzania katika masoko ya kikanda.

109. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuleta uwiano kati ya huduma zinazotolewa, kusafirisha bidhaa na miundombinu iliyopo, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kutatua changamoto ya msongamano wa malori katika mipaka. Mikakati hiyo inajumuisha upanuzi wa barabara ya kuingia kituo cha ukaguzi cha mpaka wa Tunduma kutoka njia mbili hadi nne ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15. Vilevile, kuunganisha mifumo ya forodha baina

ya Tanzania na Zambia ili kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa.

110. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, kuendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari kavu na kuharakisha upimaji wa mizigo kwa upande wa Zambia kwa kukamilisha ujenzi wa mdaki *(scanner)* wenye kasi. Utekelezaji wa mikakati hiyo utarahisisha biashara baina ya Tanzania, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine Serikali imeanza kutekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha Forodha cha Tarakea ambapo hadi Februari, 2026 uhakiki wa fidia kwa ajili ya Wananchi waliopisha mradi huo ulikuwa unaendelea. Hatua hiyo itawezesha kuimarisha utoaji wa huduma na kurahisisha biashara baina ya Tanzania na Kenya.

112. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha biashara za Watanzania, ninaelekeza Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza biashara, kuongeza uzalishaji na kuimarisha ushindani. Vilevile, katika kuboresha maeneo ya kufanyia biashara za wajasiriamali wadogo ikiwemo machinga, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitenge asilimia 5 ya mapato ya ndani ili kujenga na kuboresha miundombinu ya maeneo hayo.

113. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi ikiwemo utafutaji wa masoko. Vilevile, itaendelea kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara kupitia ubunifu na matumizi ya teknolojia ya kisasa, elimu na mafunzo ya ujuzi.

## USAFIRI NA USAFIRISHAJI

### Ujenzi

114. ***Mheshimiwa Spika***, miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa na inachangia katika kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika kuhakikisha huduma hiyo inakuwa bora, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege, vivuko na majengo ya Serikali pamoja na kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani.

*115.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara nchini, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 4,813.12 na changarawe kilomita

5,741.17. Vilevile, inaendelea kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 23,871.59.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza msongamano wa vyombo vya moto na kurahisisha usafiri, usafirishaji na upatikanaji wa huduma katika Jiji la Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya upanuzi na ujenzi wa barabara. Kwa upande wa Jiji la Dodoma, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje yenye urefu wa kilomita 112.3 ambapo barabara ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa *Dry Port* yenye urefu wa kilomita 52.3 umefikia asilimia 93 na Ihumwa *Dry Port* – Matumbulu – Nala yenye urefu wa kilomita 60 umefikia asilimia 95. Barabara hiyo itawezesha magari kutumia njia hiyo na kuendelea na safari bila kulazimika kupita katikati ya jiji na hivyo kupunguza foleni.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, miradi inayotekelezwa na Serikali ni pamoja na upanuzi wa barabara ya kilomita 5.2 kutoka njia nne hadi njia nane kati ya Ubungo na Kimara pamoja na upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8). Miradi mingine ni ujenzi wa barabara za mabasi yaendeyo haraka awamu ya tatu hadi ya tano ambao upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Jiji la Mbeya, Serikali inaendelea kufanya upanuzi wa barabara ya Igawa – Tunduma sehemu ya Uyole – Ifisi (km 29). Aidha, katika Jiji la Mwanza, Serikali imeendelea kutekeleza na kukamilisha mradi wa ujenzi wa Barabara ya Buhongwa – Kishiri – Nyamhongolo (km 12). Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uchumi wa nchi ni vema kuhakikisha miundombinu ya barabara inajengwa, inakamilika kwa wakati na kutumika katika kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji. Katika kufikia azma hiyo, Wizara ya Ujenzi isimamie ukamilishaji wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea pamoja na kuhakikisha wakandarasi waliosaini mikataba wanatekeleza na kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kuendelea kuimarisha barabara za mijini na vijijini hasa barabara za vipaumbele katika majimbo, ninaelekeza Wizara ya Fedha iimarishe vyanzo vya upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, ihakikishe fedha hizo zinapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko kama ilivyotengwa kwenye bajeti.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na upanuzi wa mtandao wa barabara, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja ya Mkili (Ruvuma); Mbangala (Mtwara); na Nguyami na Chakwale (Morogoro). Aidha, inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja makubwa 13 ambayo ni Mirumba, Mitomoni (Ruvuma); Pangani (Tanga); Simiyu (Simiyu); Mbambe (Pwani); Doma (Morogoro); Mwanjiri na Nzali (Dodoma); Suguta (Mara); Sukuma (Mwanza); Jangwani (Dar es Salaam); Kalebe (Kagera); na Kavuu (Katavi). Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja hayo, kutarahisisha mawasiliano na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa usafiri wa anga katika kuharakisha shughuli za kiuchumi na za kijamii, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Ujenzi wa kiwanja hicho umefikia asilimia 84 kwa upande wa miundombinu na asilimia 70 kwa ujenzi wa majengo. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, uzio wa usalama pamoja na barabara za viungio.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizo za Serikali zimeenda sambamba na kuhakikisha wakandarasi wazawa wanajengewa uwezo ili kumudu ushindani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hatua mahsusi iliyochukuliwa na Serikali ni pamoja na kukusanya mitaji ya kuwawezesha wakandarasi wazawa kupitia hatifungani ya Miundombinu iitwayo *Samia Infrastructure Bond.*

124. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2026, shilingi bilioni 9.09 zimekopeshwa kwa wakandarasi wazawa 87 wanaotekeleza miradi ya TARURA. Kupitia hatifungani hizo, wakandarasi wazawa wamepata mitaji ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara na hivyo kukamilisha miradi kwa wakati pamoja na kuepuka gharama za kuhudumia mradi zaidi ya muda uliopangwa.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za kimkakati ili kufungua fursa za kiuchumi na barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, wilaya na nchi jirani kwa kiwango cha lami. Vilevile, itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za mchepuko, mzunguko na mwendokasi ili kupunguza msongamano katika majiji na miji inayokua kwa kasi pamoja na kuendelea kuimarisha

miundombinu na huduma za vivuko, madaraja; na viwanja vya ndege.

**Uchukuzi**

126. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika sekta ya usafiri na usafirishaji, Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati ya reli ya *Standard Gauge Railway* (SGR). Hadi Februari, 2026 ujenzi wa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 67.85; Makutupora – Tabora (km 368) asilimia 14.54; Tabora – Isaka (km 165) asilimia 8.95; na Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 9.06.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, hatua za maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Uvinza – Malagarasi – Msongati (km 282) zinaendelea. Kama waheshimiwa wabunge mtakumbuka tarehe 16 Agosti, 2025 jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo liliwekwa na mkandarasi amelipwa malipo ya awali.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma, usafirishaji wa mizigo ulianza Juni, 2025 ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 tani 52,305 za mizigo zilisafirishwa. Kutekelezwa kwa mradi huo, kumewezesha wananchi, wafanyabiashara na watalii kusafiri

kwa haraka na hivyo kupunguza muda wa safari na kuchochea ongezeko la shughuli za kiuchumi.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usafiri wa majini, Serikali imeendelea kuongeza ufanisi wa utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kuendelea na ujenzi wa gati mbili kati ya 10 yenye urefu wa mita 500 kila moja ambao umefikia asilimia 10. Pia, inaendelea na ujenzi wa matenki 15 ya kupokelea mafuta mita za ujazo 378,000 ambao umefikia asilimia 41. Uboreshaji wa bandari hiyo utawezesha kuhudumia shehena tani milioni 60 ikilinganishwa na tani milioni 32 zinazohudumia kwa sasa.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri katika Maziwa Makuu, Serikali imekamilisha maboresho ya Bandari ya Kemondo na kuendelea na maboresho ya Bandari ya Bukoba na Mwanza Kaskazini ambayo yamefikia asilimia 99 na 75 mtawalia. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa meli ya MV New Mwanza yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mizigo tani 400. Meli hiyo iliyozinduliwa Januari, 2026 inaendelea kutoa huduma kati ya bandari ya Mwanza Kusini, Bandari ya Bukoba na Bandari za Jinja na *Port Bell* zilizopo nchini Uganda.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usalama wa watu, mali na vyombo vya usafiri, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji cha Kikanda *(Maritime Rescue Cordination Centre)* kilichopo katika Ziwa Viktoria. Vilevile, imekamilisha ununuzi wa boti maalum kwa ajili ya huduma za afya za dharura na matibabu ambayo imeanza kutoa huduma.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Kampuni ya Ndege Tanzania imeongeza mtandao wa safari na kufikia vituo 33 ikilinganishwa na vituo 26 vilivyohudumiwa mwaka 2024/2025. Kati ya vituo hivyo, vituo 16 ni vya ndani ya nchi, 14 ni vya kikanda, na vitatu ni vya kimataifa ambavyo ni Victoria Falls (Zimbabwe), Cape Town (Afrika Kusini) na Accra (Ghana). Kuongezeka kwa mtandao wa safari kumewezesha ATCL kusafirisha tani 3,500 za mizigo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Januari 2026 ikilinganishwa na tani 2,567 zilizosafirishwa mwaka 2024/2025. Aidha, abiria 845,275 walisafirishwa katika kipindi hicho.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa reli, bandari, meli, vivuko, viwanja vya ndege na uendelezaji wa bandari kavu ili kuimarisha huduma ya usafiri na usafirishaji. Vilevile, itaendelea kuboresha miundombinu ya matanki ya kupokea mafuta bandarini na maeneo ya kuhifadhi shehena.

**MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

134. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika kuendeleza Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika. Hatua hiyo, inalenga kuchochea biashara kati ya nchi zetu na kuongeza mapato ya Serikali kupitia huduma za Mkongo huo.

135. ***Mheshimiwa Spika***, Wilaya za Kilwa, Maswa, Bariadi, Sikonge, Urambo, Ushirombo, Chunya, Karagwe, Nzega na Butiama zimeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa. Hivyo kufanya jumla ya wilaya zilizounganishwa kufikia 120 kati ya 139 sawa na asilimia 86.

136. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na upanuzi wa mtandao wa mkongo wa Taifa, Serikali imekamilisha ujenzi wa minara 758

katika kata 713 kwa gharama ya shilingi bilioni 126 ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Vilevile, minara 304 imeongezewa uwezo kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G na 4G ili kuongeza kasi ya intaneti na kurahisisha shughuli za biashara na uzalishaji.

137. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa kujenga na kukamilisha minara ya simu na redio. Vilevile, itaendelea kuhakikisha wilaya zilizobaki zinaunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

## HUDUMA ZA JAMII

### Elimu

*138.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya elimu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023), mitaala iliyoboreshwa, mipango na mikakati mbalimbali. Lengo ni kuzalisha rasilimaliwatu wenye ujuzi na maarifa stahiki yatakayowezesha kumudu ushindani wa ajira na uwezo wa kujiajiri ndani na nje ya nchi.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini inaonesha kuwa wanafunzi 3,021,177 wanatarajiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2028. Jumla ya gharama zinazohitajika ni shilingi

trilioni 1.77 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 23,226; matundu ya vyoo 46,632; maabara 9,366; ajira mpya za walimu 40,192; ruzuku ya vitabu na uendeshaji pamoja na ruzuku ya mitihani na upimaji.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata nafasi ya kuendelea na masomo, kwa mwaka 2026/2027, Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri imetenga shilingi bilioni 139.28 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,193 na matundu ya vyoo 13,943. Aidha, kupitia Serikali kuu zimetengwa shilingi bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa maabara 233.

141. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Serikali imetoa shilingi bilioni 88.84 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 103 za amali. Kati ya hizo, ujenzi wa shule 27 umekamilika na zinatumika. Vilevile, hadi Februari 2026, shule 158 za Sekondari ya Chini zinatekeleza mkondo wa amali wa mitaala iliyoboreshwa ikilinganishwa na shule 41 zilizoanza mwaka 2024.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ajili ya kuboresha ufundishaji wa masomo ya amali, Serikali imepeleka walimu 150 mafunzo ya muda mfupi nchini India. Aidha, walimu 156,948 kati 172,609 kutoka shule za msingi 17,111 walishiriki mafunzo endelevu kazini.

## Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu pamoja na kukamilisha maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Lengo ni kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu katika maeneo yote na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa shule mpya za msingi 277. Vilevile, imeongeza miundombinu katika shule za msingi na sekondari zilizopo kwa kujenga madarasa 5,439, majengo ya utawala saba, mabweni 21, hosteli 26, nyumba za walimu 69, maabara 46, mabwalo matano na vituo vya walimu 70.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ukarabati, Serikali imekamilisha ukarabati wa shule za msingi 228. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa miundombinu iliyojengwa kwa nguvu za wananchi ikiwemo maboma 132 ya mabweni ya shule za sekondari, vyumba vya madarasa 697 katika shule za msingi na vyumba vya maabara 175. Aidha, ninatoa pongezi na shukrani kwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupeleka vifaa vya maabara

katika shule za sekondari 231 zikiwemo shule mpya 26 maalumu za kitaifa za sayansi za wasichana.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu na mazingira ya kujifunzia na kufundishia, uandikishaji na ufaulu wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu umeongezeka. Kwa upande wa uandikishaji, hadi Februari, 2026, wanafunzi 1,407,761 wa darasa la awali sawa na asilimia 70.8 ya lengo la 1,987,472 wameandikishwa na wanafunzi 1,681,549 wa darasa la kwanza sawa na asilimia 86.2 ya lengo la 1,950,783 wameandikishwa. Vilevile, wanafunzi 739,676 sawa na asilimia 78.89 ya lengo la 937,581 wameandikishwa kujiunga na kidato cha kwanza. Nitumie fursa hii pia kuwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka watoto wote wenye sifa shuleni. Aidha, nawaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia na kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa wanafunzi wa darasa la nne ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 86.24 mwaka 2024 hadi asilimia 88.91 mwaka 2025 na kwa darasa la saba umeongezeka kutoka asilimia 80.87 mwaka 2024 hadi asilimia 81.80 mwaka 2025.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa kidato cha pili, ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 85.41 mwaka 2024 hadi asilimia 86.93 mwaka 2025 na kidato cha nne, ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 92.37 mwaka 2024 hadi asilimia 94.98 mwaka 2025. Vilevile, kwa kidato cha sita ufaulu umefikia asilimia 99.95 mwaka 2025.

*149.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Elimu Bila Ada kwa kugharimia elimu ya awali hadi elimu ya sekondari ya juu. Hadi Februari, 2026 shilingi bilioni 383.22 kati ya shilingi bilioni 510.96 sawa na asilimia 75 zilitolewa kwa shule za msingi 18,119 na shule za sekondari 5,179.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imewezesha upatikanaji wa vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya matumizi ya walimu na wakufunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta mpakato, vifaa vya kuandikia na kuhifadhi taarifa kwa *braille*, vinasa sauti, vishkwambi vinavyotafsiri kwa lugha ya alama, vikuza sauti, kivunge cha vifaa vya kuongeza uwezo wa kuona na vifaa vya kupima usikivu. Serikali itaendelea kugharimia vifaa kwa ajili ya wanafunzi na walimu hao kwa lengo la kutoa fursa sawa katika kufundisha na kujifunza.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyuo vya VETA 64 vya wilaya ambao umefikia wastani wa asilimia 67 na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe kilichofikia asilimia 68. Hatua hii ni utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuwa na chuo cha VETA katika kila mkoa na wilaya. Lengo ni kusogeza huduma za mafunzo ya ufundi stadi karibu na wananchi ili kuongeza ujuzi, kukuza ajira, na kuongeza kasi ya maendeleo ya uchumi wa viwanda.

152. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na umuhimu wa elimu ya kati na elimu ya juu, Serikali inaendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu hiyo nchini. Kwa upande wa elimu ya juu, kwa mwaka 2025/2026 wanafunzi 170,916 wamedahiliwa katika vyuo vikuu ikilinganishwa na wanafunzi 137,781 waliodahiliwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 24.

153. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha fursa za masomo ya elimu ya kati na elimu ya juu inapatikana kwa makundi yote ya kijamii, Serikali imeendelea kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati. Jumla ya shilingi bilioni 899.21 zimetolewa katika mwaka 2024/2025 ambapo shilingi bilioni 348.77 zimetolewa kwa wanafunzi 107,541 wa mwaka wa kwanza na shilingi bilioni 550.44 imetolewa

kwa wanafunzi 177,492 wanaoendelea na masomo.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imetoa ufadhili wa shilingi bilioni 9.46 kupitia *SAMIA Scholarship* kwa wanafunzi 1,786 wenye ufaulu unaojipambanua wanaosoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati katika vyuo vikuu hapa nchini. Vilevile, imetoa ufadhili wa shilingi bilioni 5.487 kupitia *SAMIA Scholarship Extended* kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu wa kidato cha sita katika fani za sayansi waliochaguliwa kusoma Shahada ya Kwanza katika fani za Sayansi Data, Akili Unde na Sayansi Shirikishi katika vyuo bora duniani.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utoaji wa mikopo, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu katika taasisi za elimu ya juu. Katika mwaka 2025/2026 imekamilisha ujenzi wa kampasi mpya 2 na inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Kampasi nyingine 14 ambao umefikia hatua mbalimbali za ukamilishaji. Lengo ni kusogeza huduma ya elimu ya juu karibu na wananchi kwa kuhakikisha kila mkoa unakuwa na taasisi ya elimu ya juu.

## Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza afua mbalimbali za kuendeleza wabunifu na kufanya teknolojia zao kuwa bidhaa. Afua hizo ni pamoja na uwepo wa Mfuko wa *Samia Innovation Commercialization Fund* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wabunifu ambapo jumla ya shilingi milioni 667 zimetolewa katika awamu ya kwanza kwa wabunifu saba. Miongoni mwa bunifu zilizokopeshwa ni pamoja na uchakataji na usambazaji wa asali bora na mafuta ya mawese kwa ajili ya masoko ya nje pamoja na mfumo wa kudhibiti foleni katika hospitali. Vilevile, Serikali imekamilisha na kuidhinisha Mkakati wa Kitaifa wa Kuhamasisha mchango wa Diaspora katika shughuli za Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

157. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha na kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Vilevile itaendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati. Aidha, itaendelea kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**Afya**

158. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma ya elimu, Serikali imeendelea kusimamia ubora, usalama na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia zahanati hadi Taifa. Vilevile, imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba ili kuhakikisha nchi inakuwa na utoshelevu.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo zinaenda sambamba na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kuendelea kutekeleza miradi ya ujenzi 113 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya miradi hiyo, miradi 45 inatekelezwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa; miradi 11 katika Hospitali ya Taifa, Maalum na Hospitali za Kanda; miradi 9 katika vyuo vya mafunzo; na miradi 48 katika Hospitali za Halmashauri.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeajiri wataalamu 4,183 kwa utaratibu wa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani ya taasisi husika. Kati yao, watumishi 3,202 wameajiriwa kwenye Hospitali za

Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Hospitali ya Taifa Muhimbili na watumishi 981 wameajiriwa ngazi ya afya ya msingi. Pia, watumishi 1,000 wa mikataba wameajiriwa kupitia programu ya uwekezaji katika afya ya mama na mtoto Tanzania.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita katika huduma za afya umeongeza upatikanaji kwa bidhaa za afya za kipaumbele 290 katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka wastani wa asilimia 80 mwaka 2024 hadi wastani wa asilimia 89 Februari, 2026. Aidha, hadi Januari, 2026, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 209.5 kwenye vituo kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya. Pia, imetoa shilingi bilioni 33.80 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali za Halmashauri 142, vituo vya afya 184 na zahanati 184.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bingwa na bobezi, Serikali inatekeleza mikakati mahsusi ya kuongeza madaktari bingwa na bingwa bobezi. Moja ya mikakati hiyo ni kuanzisha programu ya ufadhili ya *Samia Health Super-specialization Program.* Kupitia programu hiyo, jumla ya wataalamu 1,483 wamepata ufadhili wa masomo katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** ufadhili wa masomo kwa wataalamu hao utaongeza idadi ya wataalamu watakaotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini. Aidha, kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya nchini kumewezesha wagonjwa kutoka nje ya nchi kuja nchini kwa ajili ya kupata huduma za matibabu.

*164.* ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono haya makubwa. Hakika Mheshimiwa Rais amethibitisha kwa vitendo dhamira yake njema ya kuthamini na kujali afya na utu wa Watanzania kwa kuhakikisha huduma za kibingwa na bingwa bobezi zinapatikana hapa nchini.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza uwezo wa nchi kuzalisha dawa na vifaa tiba, mifumo ya ugharimiaji wa huduma za afya, kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA, kuboresha miundombinu, kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, utafiti na kuimarisha tiba utalii.

**Mapambano Dhidi ya VVU na UKIMWI**

166. ***Mheshimiwa* Spika,** katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, jitihada zilizofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zimewezesha Taifa letu kupiga hatua kubwa katika kupunguza maambukizi mapya ya VVU, kudhibiti maradhi na vifo vitokanavyo na UKIMWI na WAVIU wengi kuishi maisha yenye afya na tija kutokana na matibabu bora ya kufubaza VVU.

167. ***Mheshimiwa Spika***, tathmini ya hali ya mwitikio dhidi ya UKIMWI imeonesha kuwa takribani watu 1,700,000 wanaishi na Virusi Vya UKIMWI. Aidha, tathmini hiyo imebaini kuwa kiwango cha watu wanaotambua hali za maambukizi ya VVU imeongezeka kutoka asilimia 91 mwaka 2024 hadi asilimia 92 mwaka 2025; WAVIU wanaotumia dawa za kufubaza VVU imeongezeka kutoka asilimia 98 mwaka 2024 hadi asilimia 98.5 mwaka 2025; na WAVIU wanaotumia dawa za ARV ambao wamefubaza VVU imeongezeka kutoka asilimia 97 mwaka 2024 hadi asilimia 98.1 mwaka 2025.

168. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo kwa WAVIU ili kuhakikisha huduma

za VVU na UKIMWI zinapatikana kwa urahisi kutoka vituo 7,805 kwa mwaka 2024 hadi vituo 8,203 kwa mwaka 2025; idadi ya mashine kubwa za kupima wingi wa VVU mwilini zimeongezeka kutoka mashine 43 mwaka 2024 hadi 50 mwaka 2025; na kuendelea kuhakikisha Dawa za kufubaza makali ya VVU zinapatikana kwa asilimia 100 ambazo hutolewa bure kwa WAVIU wote.

169. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha uwezo wa ndani katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, Serikali imeendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI. Hadi Februari, 2026, Serikali imekusanya shilingi bilioni 26.8 kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI. Hatua hii ni muhimu kwa nchi yetu kujitegemea na kuimarisha uwezo wa ndani katika kugharimia mwitikio, kinga na tiba dhidi ya VVU na UKIMWI.

170. ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia lengo la kutokomeza UKIMWI kama janga la afya ya jamii ifikapo mwaka 2030. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kushirikiana na wadau wote wa maendeleo katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kugharimia kinga, tiba pamoja na matunzo.

**Uratibu wa Masuala ya Lishe**

171. ***Mheshimiwa* Spika,** masuala ya lishe ni muhimu sana katika kuimarisha nguvukazi inayotarajiwa kutekeleza mipango na mikakati yote ya Serikali. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe (2021/2022 – 2025/2026) ambao utekelezaji wake unafikia ukomo Juni, 2026. Mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa mpango huo ni pamoja na kupungua kwa udumavu kwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 kutoka asilimia 34 hadi 30. Pia, kuajiri wataalamu 637 wa lishe na kupangwa katika mikoa yote. Vilevile, kupitia programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania, watumishi 400 wameajiriwa kwa mkataba ili kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo za lishe.

172. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kufanya maandalizi ya mpango wa muda mrefu wa lishe 2026 – 2050 ambao utekelezaji wake utashabihiana na utekelezaji wa Dira 2050. Mpango huo utatoa mwelekeo kwa wadau wote wa masuala ya lishe nchini.

## Maji

173. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya maji ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe vyote. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji katika maeneo mbalimbali nchini. Jitihada hizo zimeimarisha wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini kutoka asilimia 83.0 Desemba, 2024 hadi asilimia 85.2 Desemba, 2025 na kwa maeneo ya mijini kutoka asilimia 91.6 Desemba, 2024 hadi asilimia 92.5 Desemba 2025.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ya kimkakati inayotekelezwa ni pamoja na mradi wa maji wa miji 28 ya Tanzania Bara katika miji ya Handeni, Korogwe, Muheza, Pangani, Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Rujewa, Chunya, Njombe, Makambako, Wanging'ombe na Kiomboi. Miji mingine ni Singida, Manyoni, Mugumu, Chemba, Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Chato, Geita, Newala, Nanyamba na Tandahimba, pamoja na sehemu ya Halmashauri za Wilaya za Mtwara, Mafinga, Rorya - Tarime na Songea. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo umefikia kati ya asilimia 14 na 89.8. Kukamilika kwa miradi hiyo kutanufaisha wananchi wapatao 5,985,500 wa maeneo hayo.

*175.* ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu shilingi bilioni 329.46 umefikia asilimia 40. Mradi huo ukikamilika utaimarisha utiririshaji wa maji ya Mto Ruvu katika kipindi chote cha mwaka na kulisha mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Lakini pia, utazalisha umeme megawati 20, kuwezesha shughuli za kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa vijijini, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati yenye gharama ya shilingi bilioni 349.59. Utekelezaji wa miradi hiyo, umefikia kati ya asilimia 5 hadi 75. Kukamilika kwa miradi hiyo kutahudumia vijiji 225**.**

177. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati itakayounganishwa kwenye Gridi ya Taifa ya Maji inayohusisha kutoa maji maeneo yenye vyanzo vya uhakika kupeleka maeneo yenye uhaba wa maji. Vilevile, itaandaa Mpango Kabambe kwa lengo la kutoa mwelekeo wa muda mrefu na wa kimkakati wa kitaifa wa kusimamia, kuendeleza na kutumia rasilimali za maji kwa njia endelevu.

## URATIBU WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU

178. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa jamii ya Watu Wenye Ulemavu inaendelea kupata huduma muhimu za kuimarisha haki na ustawi wao pamoja na kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu imetoa ruzuku ya shilingi milioni 238.92 kwa vyama 13 vya Watu Wenye Ulemavu ili kuendeleza shughuli zao.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Serikali imeiwezesha Bohari ya Dawa kuzalisha na kusambaza vifaa saidizi na mafuta kinga kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imetoa chupa 105,557 za mafuta ya kujikinga na mionzi ya jua kwa watu wenye ualbino katika mikoa 24 ya Tanzania Bara. Kadhalika, imewezesha upasuaji wa saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino katika Taasisi ya Utafiti wa Saratani ya Ocean Road na Hospitali ya KCMC.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imewezesha kituo atamizi kilichopo Chuo cha Ufundi Sabasaba Singida kuimarisha ujuzi kwa wanafunzi Wenye Ulemavu. Vilevile, imeimarisha huduma ya utengamao kwa watoto wenye ulemavu hususan vichwa

vikubwa, mgongo wazi na wenye usonji ili kupunguza madhila yanayotokana na kuwahudumia watoto hao.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imetoa huduma ya afya ya macho kwa kufanya uchunguzi kwa watu 91,227 ambapo watu 11,047 waliobainika kuwa na matatizo ya macho walipatiwa miwani. Vilevile, imetoa vifaa saidizi kwa Watu Wenye Ulemavu katika Mikoa ya Kigoma, Ruvuma, Mbeya, Tanga, Shinyanga, Mara na Dodoma ambapo watu 6,618 wamenufaika.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha mfumo wa uratibu wa Watu Wenye Ulemavu, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuratibu na Kusimamia Watu Wenye Ulemavu. Mfumo huo unapokea taarifa binafsi na takwimu zote sahihi za Watu Wenye Ulemavu zitakazowezesha kutambua mahitaji yao kwa ajili ya kupanga mipango mikakati na bajeti. Maafisa TEHAMA na Ustawi wa Jamii kutoka Halmashauri zote za Mikoa 14 ya Mara, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Kigoma, Katavi, Tabora, Dodoma, Ruvuma, Mtwara, Lindi na Njombe wamejengewa uwezo kuhusu mfumo huo.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha huduma kwa Watu Wenye Ulemavu kwa kuratibu afua za ulinzi na ustawi, kuratibu programu za uwezeshaji kiuchumi na kuendeleza ujuzi. Vilevile, Serikali itaandaa utaratibu maalumu wa kuwawezesha na kuwasaidia Watu Wenye Ulemavu pamoja na wale wanao wahudumia.

## URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI BUNGENI

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuratibu shughuli zake Bungeni. Moja ya shughuli zilizofanywa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la 13 ni kuratibu uwasilishaji wa Hotuba ya Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hotuba aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la 13 na kujadiliwa na Bunge. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa, Serikali inaahidi kuendelea kutekeleza ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, miswada miwili ilisomwa kwa mara ya kwanza na nyaraka muhimu za kimkakati ziliwasilishwa na kuidhinishwa na Bunge. Nyaraka hizo ni pamoja na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027-

2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027– 2030/2031), Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati wa 2026/2027- 2028/ 2029. Aidha, maswali ya msingi 146, maswali ya nyongeza 482 na maswali ya papo kwa papo saba yaliulizwa na wabunge na kujibiwa na Serikali.

## UCHAPAJI WA NYARAKA ZA SERIKALI

186. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi na utoaji huduma za uchapishaji wa nyaraka za Serikali, mikakati mbalimbali imetekelezwa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuiongezea hadhi iliyokuwa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** mabadiliko hayo yameenda sambamba na kuimarisha Wakala huo kwa kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwanda cha uchapishaji, kununua na kufunga mashine mpya nane za uchapishaji. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala na uzio ambao umefikia asilimia 78.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuzikumbusha Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi, Wakala na Idara za Serikali zinazojitegemea kuchapa nyaraka za Serikali kupitia Wakala huo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, Tamko Na. 2 la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 750A la tarehe 15 Agosti, 2014 na Waraka wa Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali wa tarehe 14 Februari, 2024.

**ULINZI NA USALAMA**

189. ***Mheshimiwa Spika,*** ulinzi wa mipaka ya nchi yetu ni suala muhimu katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kufanya shughuli za uzalishaji mali bila bughudha yoyote. Pamoja na ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshiriki katika ulinzi na usalama kikanda na kimataifa.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi letu lilishiriki katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani kikanda na kimataifa. Operesheni hizo ni pamoja na zinazoendeshwa na Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika ya Kati, Lebanon na Sudan Kusini. Aidha, ushiriki katika operesheni hizo umeiwezesha nchi yetu kujenga uwezo, kuimarisha diplomasia ya ulinzi, uhusiano na

kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa kulinda usalama wa raia na mali zao, Serikali imeendelea kuimarisha vyombo vya usalama. Eneo mojawapo lililopewa kipaumbele ni kulijengea uwezo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vifaa na kujenga vituo vipya vya zimamoto.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 vifaa na mitambo ya kuzima moto yenye thamani ya dola za Marekani milioni 100 imenunuliwa na kusambazwa mikoa yote nchini. Aidha, imejenga vituo saba vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Katavi, Geita, Manyara, Njombe na Kagera.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la utambuzi wa raia limeendelea kuwa kipaumbele cha Taifa letu kutokana na umuhimu wake katika ulinzi na usalama lakini pia utoaji wa huduma za jamii. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Januari 2026, Serikali imesajili wananchi 435,953 na hivyo kufikisha idadi ya wananchi 26,477,044 waliosajiliwa nchini sawa na asilimia 84.1 ya watu wote wenye sifa za kusajiliwa. Aidha, taasisi 138 za umma na binafsi zimeunganishwa katika mfumo wa usajili na utambuzi ili kurahisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika zama za sasa ambapo Dunia inakumbwa na changamoto za kiusalama, ni muhimu kwa wananchi wote bila kujali itikadi za dini na siasa kulinda rasilimali za Taifa, kuongeza uzalendo, kupinga chuki na vitendo vyovyote vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa Taifa. Jitihada hizo zitaepusha maadui wanaoweza kujipenyeza na kuhatarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu pamoja na maendeleo.

195. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, nitoe wito kwa wazazi na walezi kuendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi za elimu na dini katika kuimarisha malezi ya watoto na vijana. Misingi imara ya maadili, uzalendo na matumizi sahihi ya teknolojia na utandawazi yatawawezesha watoto na vijana kufikia ndoto zao pamoja na kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa.

196. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu na usalama wa raia na mali zao. Aidha, itaendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia zana, vifaa na rasilimaliwatu.

## KUKUZA FURSA ZA AJIRA NA UJUZI

197. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuratibu uzalishaji wa fursa za ajira nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kubaini fursa kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2026, fursa za ajira 625,273 zilizalishwa. Kati ya ajira zilizozalishwa, ajira 242,656 za wazawa zilitokana na vibali 12,549 vilivyotolewa kwa wageni sawa na uwiano wa mgeni 1 kwa wazawa 19 ikilinganishwa na uwiano wa mgeni 1 kwa wazawa 10 kama ilivyoainishwa katika Sheria ya kuratibu Ajira za Wageni, Sura 436.

*199.* ***Mheshimiwa Spika****,* katika hatua nyingine, Serikali imewezesha upatikanaji wa fursa za ajira 6,367 kwa Watanzania katika nchi za Saudia, Qatar, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu. Nchi nyingine ni pamoja na Bahrain, Denmark, Ujeruman, Kuwait, Poland, Bosnia, Sweden, Romania, Guyana, Marekani, Mauritius na Ireland.

200. ***Mheshimiwa Spika****,* aidha, Agosti, 2025, Serikali ilizindua Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Soko la Ajira ambao unatumika

kukusanya, kuchambua na kutangaza taarifa za soko la ajira. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza Mwongozo wa Uratibu wa Mawakala Binafsi wa Ajira wa Mwaka 2025 na kuendelea kuingia makubaliano na nchi husika ili kuhakikisha Watanzania wanafanya kazi za staha kwa kipato stahiki.

201. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuwezesha uzalishaji wa fursa za ajira, Serikali imeendelea kuhakikisha nguvukazi inapata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Ili kufikia azma hiyo, katika mwaka 2025/2026 Serikali imewezesha mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya uanagenzi kwa vijana 5,746 katika vyuo na taasisi za mafunzo 46. Vilevile, imetoa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wakulima na wasindikaji wadogo 1,065 wa mazao mbalimbali ili kupunguza upotevu na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

202. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, imewezesha mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa njia ya utarajali kwa vijana 2,500 na mafunzo maalum ya kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwa vijana 7,826. Aidha, Serikali imesaini hati ya ushirikiano na Serikali ya Japan kuhusu utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa vijana katika kampuni mbalimbali za ujenzi nchini Tanzania na Japan.

203. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kisera kwa lengo la kukuza fursa za ajira jumuishi, endelevu na zenye staha kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi yanayotokea duniani.

## MASUALA YA KAZI NA WAFANYAKAZI

204. ***Mheshimiwa Spika,*** watumishi wa umma ni nguzo ya msingi katika utekelezaji wa sera, dira, mipango na mikakati ya Serikali. Kwa kutambua umuhimu wa watumishi wa umma, Serikali ya Awamu ya Sita baada ya kuingia madarakani hadi Machi, 2026 imepandisha vyeo/madaraja jumla ya watumishi 662,707 kati ya 678,115 waliopo kwenye orodha ya walipwa mishahara. Kadhalika, katika kipindi hicho, Serikali imebadilisha kada/miundo watumishi 42,515 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.52. Vilevile, imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 148,137 yenye jumla ya shilingi bilioni 248.52 na imeajiri watumishi wapya 155,008. Aidha, Serikali itaendelea kuajiri, kupandisha vyeo na madaraja, kuongeza mishahara na kuwaendeleza watumishi ndani ya utumishi wa umma kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

205. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, mwenendo wa malipo ya mishahara unaonesha kuwa lipo kundi la watumishi wapatao 7,447 ambao wanalipwa mishahara binafsi isiyoendana na majukumu wanayofanya. Hadi tarehe 26 Machi, 2026 watumishi hao wamelipwa mishahara binafsi kwa gharama ya shilingi bilioni 14.34.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na hali hiyo, Serikali itafanyia kazi masuala yafuatayo: ***Mosi,*** kuwianisha mishahara ya watumishi wa umma pamoja na kupunguza tofauti kubwa ya viwango vya mishahara katika utumishi wa umma na sekta binafsi. ***Pili,*** kuhuisha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 na kanuni zake kuhusu idhini ya utoaji wa kibali cha mshahara binafsi. ***Tatu,*** kuhuisha Waraka unaohusu Watumishi watakaobadilishwa kazi ili kuendana na mahitaji ya sasa. Vilevile, kufanya mapitio ya Waraka kuhusu utaratibu wa kushughulikia maombi ya mishahara binafsi kwa watumishi wa umma.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kukamilisha na kutangaza Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi kilichoongezeka kwa viwango tofauti kwa kuzingatia sekta. Utekelezaji wa amri hiyo ulianza rasmi Januari, 2026. Aidha, katika kuimarisha utekelezaji wa amri hiyo,

Serikali inaendelea kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kote nchini.

208. ***Mheshimiwa Spika***, watoto ni kundi maalumu ambalo linahitaji afua mahsusi ili kuhakikisha kila mtoto anapata haki zake kama zilivyoainishwa kwenye sheria za nchi pamoja na mikataba ya kimataifa. Hatua mojawapo iliyochukuliwa na Serikali ni kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Mtoto (2025/2026 – 2030/2031).

209. ***Mheshimiwa Spika***, mkakati huo ni chachu ya kulinda haki ya mtoto dhidi ya utumikishwaji katika kazi zinazoweza kuathiri afya, makuzi na maendeleo ya kielimu na kijamii. Pamoja na mambo mengine, unalenga kukuza uelewa wa jamii kuhusu madhara ya utumikishwaji wa mtoto na kuhamasisha ushiriki wa wadau wote katika kulinda haki za mtoto.

210. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi na waajiri kwa kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Majadiliano baina ya Serikali, Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Aidha, itaandaa Mwongozo wa Usajili, Usimamizi na Uratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri na Mashirikisho; na Kuratibu utekelezaji wa

Programu ya Nchi ya Kazi za Staha (2025/2026 – 2029/2030).

**USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI**

211. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhakikisha maeneo ya kazi yanakuwa na mifumo ya kudhibiti athari za vihatarishi ili kupunguza ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na kazi kwa kufanya kaguzi mbalimbali. Hadi Februari, 2026, kaguzi maalum 196,701 zimefanyika katika maeneo ya viwanda, migodi na sekta ya usafirishaji na kuchukua hatua stahiki kwa maeneo yaliyobainika kuwa na changamoto. Vilevile, imefanya uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi 289,611 na kutoa ushauri stahiki kwa wafanyakazi 123,802 waliobainika kuwa na changamoto mbalimbali.

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuhakikisha maeneo ya kazi yanaendelea kuwa salama kwa wafanyakazi kwa kuendelea kusimamia sheria, kanuni na miongozo ya usalama mahali pa kazi. Vilevile, itaendelea kuimarisha uwezo wa wataalamu na kitaasisi katika kushughulikia masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

## MAENDELEO YA VIJANA

213. ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunatambua kuwa, vijana ni nguvukazi muhimu ya kujenga uchumi wa Taifa letu. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kuhakikisha vijana wa Tanzania wanawezeshwa kiuchumi, kijamii na kielimu ili kujipatia ajira na kutumia uwezo wao kikamilifu kuchangia maendeleo ya Taifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeanzisha Wizara maalumu inayoshughulikia masuala ya vijana ili kuwapa sauti ya kuwasilisha mawazo yao ambayo yatajumuishwa kwenye mipango ya maendeleo ya nchi.

214. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukuza majadiliano ya Kitaifa ya vijana, Serikali iliratibu kongamano la wajasiriamali na bodaboda lililofanyika tarehe 8 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam na kuwakutanisha washiriki zaidi ya 1,200. Kupitia kongamano hilo, vijana walipata fursa ya kuwasilisha changamoto zao ambazo zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi na Serikali.

215. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuratibu masuala ya maendeleo ya vijana ikiwemo kuwawezesha kiuchumi, kusimamia ukuzaji biashara zao, na kuimarisha ustawi na makuzi ya vijana.

## HUDUMA ZA KINGA YA JAMII

*216.* ***Mheshimiwa Spika,*** ni ukweli usiopingika kuwa, huduma ya kinga ya jamii ni muhimu sana kwa mustakabali wa ustawi wa jamii yoyote. Ukweli huo ndio msingi wa hatua na mikakati yote inayotekelezwa na Serikali katika kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa afua mbalimbali za Kinga ya Jamii nchini. Mikakati hiyo inatekelezwa kwa lengo la kuboresha huduma za Kinga ya Jamii.

217. ***Mheshimiwa Spika***, moja ya mikakati hiyo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya Mwaka 2023 ambayo imezinduliwa rasmi tarehe 9 Februari, 2026. Sera hiyo inalenga kuwawezesha wananchi kuishi katika viwango vinavyokubalika kimataifa na kutumia uwezo wao kuboresha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kuimarisha ustawi wa wastaafu kwa kuboresha kiwango cha chini cha pensheni ya kila mwezi kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 250,000 kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Aidha, Serikali imeboresha muda wa utoaji wa huduma kwa wanachama ambapo mafao yanalipwa ndani ya siku 30, na pensheni inalipwa tarehe 25 ya kila mwezi.

*219.* ***Mheshimiwa Spika***, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kuimarika ambapo hadi Februari, 2026 ilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi trilioni 24.60. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

220. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2026 Mfuko wa NSSF umesajili wanachama 226,799; umekusanya michango ya shilingi trilioni 1.22; na kulipa mafao ya shilingi bilioni 531.07. Kwa upande mwingine, Mfuko wa PSSSF umesajili wanachama 21,792, umekusanya michango ya shilingi trilioni 1.272 na kulipa mafao ya shilingi bilioni 883.26. Aidha, mfuko wa WCF umesajili waajiri wapya 1,619 na umelipa madai ya mafao ya shilingi billioni 10.14 kwa wanufaika 1,991 walioumia au kuugua. Vilevile, umelipa fidia kwa wategemezi wa waliofariki kutokana na kazi kwa mujibu wa mikataba yao ya kazi.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupanua wigo wa Kinga ya Jamii kwa wananchi waliojiajiri katika sekta isiyo rasmi, Serikali imezindua mpango maalum wa wananchi waliojiajiri. Mpango huo uitwao 'Hifadhi Scheme' unatarajiwa kuwafikia mamilioni ya Watanzania waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa pensheni.

222. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mpango huo ni sehemu ya mkakati wa kujenga mfumo jumuishi wa kinga ya jamii nchini. Hadi kufikia tarehe 28 Februari 2026, Mfuko ulikuwa na wanachama 601,434 kupitia Skimu ya Uchangiaji wa Hiari.

223. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuboresha huduma za Kinga ya Jamii nchini. Vilevile, itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya usajili wa wanachama wapya na kuhamasisha ushiriki wa wananchi waliojiajiri kupitia sekta binafsi.

## URATIBU WA MASUALA YA MAHUSIANO

224. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, mshikamano, ustahimilivu na maendeleo jumuishi, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliikasimisha Ofisi ya Waziri Mkuu jukumu la kuratibu masuala ya mahusiano nchini. Jukumu hilo linahusisha kuratibu makundi ya kijamii ikijumuisha wadau wa siasa, taasisi za dini, asasi za kiraia, na mashirika yasiyo ya kiserikali.

225. ***Mheshimiwa Spika***, ili kufikia maono hayo, mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa

Uratibu wa Mahusiano Baina ya Serikali na Makundi ya Kijamii wa Mwaka 2026. Vilevile, itaandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa Kuhusu Mahusiano na Kuratibu Afua na Ushirikishwaji wa Wadau wa Mahusiano Nchini. Aidha, Serikali itafanya tathmini ya hali ya mahusiano nchini na kuendelea kukutana na wadau kwa lengo la kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na Makundi ya Kijamii.

## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

226. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha uratibu na utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji 75 zinazomilikiwa na Serikali na sekta binafsi. Hadi Januari, 2026, mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa mikopo na dhamana zenye thamani ya shilingi trilioni 1.69 kwa wanufaika 422,921. Mifuko na programu hizo pia, zimetoa ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 598.72 kwa wanufaika 6,454,580.

227. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kwa kutafuta fursa za biashara na masoko nje ya nchi ili waweze kukuza biashara zao. Katika mwaka 2025/2026, Serikali imewezesha wajasiriamali wadogo na wa kati 315 kushiriki maonesho ya wajasiriamali wadogo na wa kati wa Jumuiya

ya Afrika Mashariki yajulikanayo kama Nguvukazi/ Juakali yaliyofanyika Novemba, 2025 Nairobi, Kenya.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha kaya masikini, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ilitoa shilingi bilioni 43.53 ambazo zilihawilishwa kwa kaya za walengwa 896,746 katika maeneo 186 nchini hadi Februari 2026. Aidha, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele cha mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi kutoka katika kaya masikini ambapo kwa mwaka 2025/2026 wanafunzi 3,179 wa kaya maskini kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walinufaika na utaratibu huo.

229. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri, hadi Februari, 2026, shilingi bilioni 130.42 zimekopeshwa kwa vikundi 12,997 vya vijana, wanawake na Watu Wenye Ulemavu. Aidha, Serikali imeimarisha usimamizi wa mikopo hiyo na hivyo kuwezesha kiasi cha shilingi bilioni 49.11 kurejeshwa.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu ushiriki wa Watanzania katika fursa zinazotokana na shughuli za kiuchumi zinazotekelezwa katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Januari, 2026 jumla ya kampuni 389 za

makundi maalum kati ya kampuni 166,477 zilipata zabuni za Serikali.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakandarasi wa kitanzania walishiriki katika kutekeleza miradi 5,177 sawa na asilimia 97.1 ya miradi iliyotekelezwa. Miradi hiyo ina thamani ya shilingi bilioni 14 ambapo shilingi bilioni 10 sawa na asilimia 72.17 zilienda kwa kampuni za ndani na shilingi bilioni 4 sawa na asilimia 27.83 zilienda kwa Kampuni za kigeni.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ajira kwa Watanzania walioshiriki katika miradi ya kimkakati na uwekezaji ziliongezeka kutoka 217,808 mwaka 2024/2025 hadi ajira 286,219 mwaka 2025/2026. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 31.4.

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha mifuko na programu za uwezeshaji wananchi zinazomilikiwa na Serikali pamoja na za sekta binafsi. Aidha, itaendelea kufanya mapitio kwa lengo la kuboresha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ya Mwaka 2023. Hatua hiyo itawezesha kuongeza idadi ya wananchi wanaonufaika na uwekezaji wa miradi ya kimkakati. Vilevile, itakamilisha maandalizi ya Mpango wa Kunusuru Kaya

Maskini Awamu ya Tatu na kutambua walengwa wapya wa mpango kwenye maeneo ya utekelezaji.

## MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa kwa kuweka mkazo kwenye kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Aidha, imeendelea kufanya uchunguzi ili kudhibiti vitendo vya rushwa. Kutokana na jitihada hizo, kiasi cha shilingi bilioni 60.231 zimeokolewa.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 60.038 zilirejeshwa Serikalini na shilingi milioni 192.88 zilirejeshwa kwenye miradi, huduma na wananchi waliodhulumiwa. Matokeo ya juhudi hizo yameleta nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika utumishi wa umma, biashara na uwekezaji.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na matokeo hayo mazuri, kwa mara nyingine ninaelekeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuweka mikakati ya kuzuia vitendo vya rushwa badala ya kusubiri vitendo hivyo kusababisha madhara. Wahenga walisema "***tahadhari kabla ya hatari"*** wakiweka msisitizo wa kuzuia badala ya kusubiri athari zitokee.

237. ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya kuendelea kutekeleza kikamilifu suala la usimamizi wa tamko la rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma, baadhi ya maeneo yana mianya ya ukosefu wa maadili. Maeneo hayo ni pamoja na ununuzi wa umma, makusanyo ya mapato, makadirio ya kodi, mikataba, utoaji wa leseni za madini, sekta ya ardhi, wajumbe wa zabuni, ukaguzi na udhibiti.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya watumishi wa maeneo hayo hawawajibiki na sheria ya maadili. Kwa mara nyingine, ninaelekeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ifanye marekebisho ya Sheria na Kanuni ili kujumuisha watumishi hao kujaza fomu ya tamko la rasilimali na madeni.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa kwa kuziwezesha taasisi za utawala bora, maadili na uwajibikaji kutekeleza majukumu yao. Vilevile, itaendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuongeza ufanisi kwenye kukabiliana na rushwa hapa nchini.

## MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

240. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na dawa za kulevya kupitia mikakati mbalimbali. Mikakati hiyo inalenga kupunguza upatikanaji, uhitaji, madhara na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na dawa za kulevya.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia utekelezaji wa mikakati hiyo, Serikali imefanikiwa kukamata kilogramu 360,479.9 za aina mbalimbali za dawa za kulevya zilizohusisha watuhumiwa 5,776. Dawa zilizokamatwa ni pamoja na bangi, mirungi, skanka, *heroin, cocaine*, dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali bashirifu.

242. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu ambapo vilabu 15,186 vimeanzishwa kwa ajili ya kupinga rushwa na dawa za kulevya. Vilevile, imetoa elimu kwa wadau 4,343,248 wakiwemo wanafunzi, viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, vyombo vya ulinzi na usalama, Mahakama, watumishi wa afya, wasanii, maafisa wa viwanja vya ndege na wafungwa.

243. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutoa huduma za tiba na utengamao kwa waraibu 18,048 ambao wamesajiliwa katika vituo 20 vya kutolea tiba ambapo waraibu 4,790 wapo kwenye matibabu. Vilevile, Serikali imeendelea kusimamia uendeshaji wa nyumba maalum za upataji nafuu 77 zinazotoa huduma za utengamao na unasihi kwa waraibu wa dawa za kulevya. Aidha, waraibu 250 waliopata nafuu wamepata mafunzo ya amali katika vyuo vya VETA na Don Bosco ili waweze kujitegemea kiuchumi.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine ya kusaidia waraibu wa dawa za kulevya, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao katika eneo la Itega, Dodoma ambao umefikia asilimia 45. Kituo kitakapokamilika, kitatoa huduma za matibabu, urekebishaji wa tabia pamoja na programu za kuwawezesha waathirika kurejea katika jamii wakiwa na uwezo wa kujitegemea.

245. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na dawa za kulevya na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

**URATIBU WA MAAFA**

246. ***Mheshimiwa Spika,*** katika uratibu wa maafa, Serikali imeanzisha mfumo wa kidijitali wa mawasiliano *'Call Center'* katika Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura. Mfumo huo unawezesha wananchi kupiga simu bure kupitia namba 190 kwa ajili ya kutoa taarifa za matukio ya maafa na kupata elimu kuhusu masuala ya maafa.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeandaa Mfumo wa Ramani za Vihatarishi vya Majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa za maeneo hatarishi kwa majanga. Mfumo huo unalenga kuwawezesha wadau kutekeleza shughuli za maendeleo kwa kuzingatia vihatarishi vya majanga.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imeratibu operesheni ya kukabiliana na tukio la moto katika Hifadhi ya Misitu Asilia ya Mlima Hanang. Aidha, imetoa misaada ya kibinadamu kwa kaya zilizoathirika.

249. ***Mheshimiwa Spika,*** misaada ya kibinadamu iliyotolewa katika operesheni hizo ina thamani ya shilingi bilioni 1 na inajumuisha chakula na vifaa vya malazi, usafi na ujenzi. Aidha, Serikali imeratibu operesheni ya kukabili

maafa na kutoa huduma za kibinadamu katika maporomoko ya udongo kwenye Mgodi Mdogo wa Dhahabu wa Nyandolwa Mkoani Shinyanga.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa maafa ili kuongeza ustahimilivu wa jamii dhidi ya majanga kwa kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati ya kupunguza vihatarishi vya maafa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**UTAWALA BORA NA SHERIA**

251. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusimamia utawala wa sheria unaozingatia misingi ya utawala bora na haki za binadamu, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kutunga sera, kufanya maboresho ya sheria, miongozo na kuandaa mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha utoaji wa haki na kuinua ustawi wa wananchi.

*252.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali imekamilisha kutafsiri na kutangaza Sheria Kuu 433 ambazo ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya kutumia Lugha ya Kiswahili kwenye utoaji wa haki. Halikadhalika, sheria 13 zilizotungwa katika Lugha ya

Kiswahili zimetafsiriwa kwenda katika Lugha ya Kiingereza.

253. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Serikali itaimarisha sekta ya sheria kwa kusogeza huduma za kimahakama, mashtaka, msaada wa kisheria hususan kwenye usuluhishi wa migogoro mbalimbali ikiwemo ya ardhi. Vilevile, itasimamia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sekta ya Sheria nchini.

## HOJA ZILIZOWASILISHWA NA MAMLAKA ZA UKAGUZI, UDHIBITI NA UCHUNGUZI

254. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuziwezesha taasisi zetu za Udhibiti, Ukaguzi na Uchunguzi kwa kufanya mabadiliko ya sheria mbalimbali ili kuziongezea nguvu, bajeti, rasilimaliwatu na vitendea kazi. Hatua hizo zimeziwezesha taasisi za udhibiti kutekeleza kikamilifu majukumu yao na kuwasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Machi, 2026.

255. ***Mheshimiwa Spika***, kaguzi zilizofanyika zimewezesha kubaini mapungufu katika usimamizi wa matumizi ya rasilimali za Serikali na kujua thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo. Vilevile, zimewezesha kuimarisha uwajibikaji, kuimarisha taasisi na uwazi katika matumizi, ufuatiliaji na kuchukua hatua stahiki. Aidha, Serikali imepokea hoja na mapendekezo yaliyowasilishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma kwa ajili ya kuzifanyia kazi. Nitumie fursa hii kulihakikia Bunge lako tukufu kwamba, Serikali itafanyia kazi hoja zote ili kuleta ufanisi wa utendaji wa Serikali.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawaelekeza Maafisa Masuuli wote wa taasisi zote za umma zenye hoja kujibu hoja hizo na kufanyia kazi mapendekezo kwa mujibu wa sheria. Katika maeneo ambayo ukaguzi umebaini wizi wa fedha na mali za umma au hujuma yoyote, ninaelekeza vyombo vyetu vya dola na mamlaka za nidhamu kufanya uchunguzi na kuchukua hatua stahiki za kisheria, kinidhamu na kiutumishi kwa wote wataobainika kuhusika.

## MFUMO WA URATIBU WA MALALAMIKO YA WANANCHI

257. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuhakikisha malalamiko ya wananchi yanapatiwa ufumbuzi kwa wakati. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mfumo wa e-Mrejesho na kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Mawasiliano na Simu ili kuwawezesha wananchi kuwasilisha kero, kupata ufafanuzi na kutoa mrejesho kuhusu masuala mbalimbali kupitia namba 190 na baruapepe ya malalamiko@pmo.go.tz.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** kituo hicho kinafanya kazi kama ngazi ya rufaa kwa changamoto ambazo hazijatatuliwa katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Wizara. Hatua hii itaimarisha uwajibikaji na ushughulikiaji wa kero, malalamiko na mrejesho kutoka kwa wananchi.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe wito kwa watumishi wa Serikali hususan Wizara za Kisekta, Taasisi, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali Mitaa kuimarisha mfumo wa kushughulikia kero za wananchi ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuwatembelea, kuwasikiliza na kuandaa jedwali na taarifa kuonesha namna walivyotatua kero za wananchi kila mwezi

## MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia mikakati na mipango ya kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo zinajumuisha kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, kuhamasisha upandaji miti, kuendeleza uwekezaji katika biashara ya kaboni na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni kama nyenzo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha Taifa na wananchi wananufaika na fursa zitokanazo na biashara hiyo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kusajili na kutekeleza miradi 92 kupitia sekta mbalimbali ikiwemo hifadhi ya misitu, nishati jadidifu na kilimo endelevu. Aidha, Halmashauri 24 kati ya 184 zinanufaika na utekelezaji wa miradi ya biashara hiyo.

262. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuhamasisha upandaji miti kupitia kampeni na programu mbalimbali na kuendelea kusimamia na kuratibu biashara ya kaboni. Vilevile, itaendelea

kutekeleza mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia kilimo himilivu, uhifadhi wa vyanzo vya maji, mifumo ya tahadhari ya majanga na mipango ya kupunguza athari za ukame, mafuriko na mabadiliko ya hali ya hewa.

## UCHUMI WA BULUU

263. ***Mheshimiwa Spika,*** Uchumi wa Buluu ni moja ya maeneo mapya ya kimkakati yanayolenga kukuza uchumi wa Taifa kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, maziwa, mito na maeneo oevu. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za Uchumi wa Buluu kupitia makongamano ya kitaifa. Aidha, imewajengea uwezo wataalam kuhusu usimamizi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia utekekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ili kuhakikisha nchi inanufaika na rasilimali za Uchumi wa Buluu na kutekeleza programu na miradi jumuishi ya kimkakati itakayokuwa chachu ya ukuaji wa uchumi kwa maendeleo endelevu.

## UJENZI WA MJI WA SERIKALI

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba. Hadi Februari, 2026 majengo 15 yameanza kutumika na ujenzi wa majengo 14 unaendelea. Katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kukamilisha majengo yaliyosalia pamoja na miundombinu ikiwemo ya maji na mawasiliano.

## MUUNGANO

*266.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili. Katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuimarisha uratibu wa Masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uratibu huu umefanywa kupitia vikao vya kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia masuala ya muungano.

267. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu, upekee na fursa za Muungano. Vilevile, itaendelea kutunza na kuenzi

tunu hii adhimu ya muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili.

## USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

268. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza sera ya mambo ya nje ambayo imekuwa nyenzo ya kuchochea maendeleo ya Taifa kwa kuimarisha diplomasia ya uchumi na kuendeleza ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa. Aidha, imeendelea kukuza biashara, kufungua masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi na kutangaza fursa za utalii na kuongeza ushawishi wa Tanzania katika majukwaa ya kikanda na kimataifa.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ushirikiano wa kimataifa, Tanzania imeendelea kuimarisha ushiriki wake kwenye majukwaa ya kimataifa kwa kuratibu na kushiriki katika mikutano ya ngazi ya juu iliyofanyika sehemu mbalimbali duniani. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Italia. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliofanyika Jijini Addis Ababa - Ethiopia uliongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

270. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika Jijini New York – Marekani. Katika mkutano huo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa *Dkt*. Philip Isdor Mpango. Pia, Tanzania ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki uliofanyika Jijini Malabo nchini Guinea ya Ikweta. Katika mkutano huo, ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa *Balozi Dkt.* Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

271. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa ushirikiano wa kikanda, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 45 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Agosti, 2025 nchini Madagascar. Katika mkutano huo, Tanzania ilishawishi utekelezaji wa maazimio ya kikanda kuhusu sekta ya nishati *(Mission 300).* Vilevile, Tanzania iliratibu na kuongoza Mkutano wa 27 wa Kamati ya Mawaziri wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama uliofanyika mwezi Julai, 2025 Jijini Dar es Salaam.

272. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano ya kikanda na kimataifa umeiwezesha nchi yetu kueleza

misimamo yake kwenye masuala mbalimbali yenye maslahi kimataifa na kuainisha vipaumbele vyake kwenye majukwaa hayo. Aidha, Serikali imetumia majukwaa hayo kutangaza mazingira wezeshi na fursa za biashara na uwekezaji katika sekta za kipaumbele ikiwemo nishati, kilimo, viwanda, miundombinu, Uchumi wa Buluu na uchumi wa kidijitali.

273. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ikiwemo kukuza upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, kuvutia uwekezaji na kukuza utalii. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu na ushirikiano wa uwili pamoja na ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya Taifa, pamoja na kustawisha diplomasia ya kisiasa na kujenga uhusiano wa karibu na nchi washirika kwa manufaa ya pande zote.

## MAENDELEO YA MICHEZO

*274.* ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania inaendelea na maandalizi ya kuwa mwenyeji katika mashindano ya AFCON 2027. Maandalizi hayo yanahusisha ujenzi na ukarabati wa viwanja pamoja na miundombinu wezeshi ikiwemo

ujenzi wa Uwanja wa Arusha uliofikia asilimia 75; ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa uliofikia asilimia 95; na ujenzi wa Uwanja wa Dodoma uliofikia asilimia 4.

275. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Meja Jenerali Isamuhyo, *Gymkhana Club* na Shule ya Sheria Tanzania kwa ajili ya mazoezi. Aidha, inaendelea na ujenzi wa Viwanja vya Farasi, *Gymkhana Annex* na *Leaders Club*.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mashindano ya wanafunzi kitaifa, kikanda na kimataifa, Serikali imeratibu michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA pamoja na kuwezesha ushiriki wa wanafunzi katika mashindano ya *CAF Schools Championship* yaliyofanyika Accra nchini Ghana. Vilevile, imeratibu ushiriki kwenye Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wanafunzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Agosti, 2025 nchini Kenya.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mashindano ya *CAF Schools Championship,* Tanzania ilipata ubingwa kwa upande wa wavulana. Mashindano hayo ya wanafunzi ni msingi wa upatikanaji wa wachezaji mahiri wa timu kubwa na timu za vijana wa chini ya miaka 15, 17 na 20 nchini.

278. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii pia, kulipongeza Shirikisho la Mchezo wa Mpira wa Miguu Tanzania kwa uongozi, uratibu na usimamizi mzuri wa mchezo huo hapa nchini. Kupitia uongozi huo, kwa mara ya kwanza Tanzania imefanikiwa kuingiza vilabu vinne kwa pamoja katika hatua ya makundi ya mashindano ya Klabu Bingwa na Shirikisho Barani Afrika. Vilabu hivyo ni Klabu ya Michezo Yanga (wananchi), Klabu ya Michezo Simba (wenye nchi), Klabu ya Michezo Azam (wana lambalamba) na Klabu ya Michezo Singida (wana kilemankundi).

279. ***Mheshimiwa Spika,*** ni dhahiri kuwa mafanikio katika mchezo wa mpira wa mguu na michezo mingine kwa ujumla ni matokeo ya uwekezaji na hamasa inayotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio hayo, siyo tu yanaleta burudani kwa mashabiki, bali yanatoa fursa ya ajira na uwekezaji hapa nchini.

280. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu ushiriki wa Tanzania katika michezo ya kimataifa na maandalizi ya AFCON 2027 ili kuacha urithi endelevu wa michezo, ajira, utalii na heshima ya Taifa. Aidha, itaendelea kuimarisha ushiriki wa wanafunzi katika michezo ili kuibua na kukuza vipaji vyao.

## MAENEO YA MSISITIZO

281. ***Mheshimiwa Spika,*** nimeelezea kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa mwaka 2025/2026 na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2026/2027. Ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, ninaomba nitumie fursa hii kutoa msisitizo kwenye maeneo mahsusi kama ifuatavyo:

**Mosi:** Kuanza utekelezaji wa Dira 2050 kupitia Mpango na Bajeti iliyoandaliwa. Kila sekta ihakikishe rasilimali za Taifa zinaelekezwa katika maeneo yenye tija na matokeo makubwa ili kupunguza utegemezi kutoka nje. Vilevile, kuendelea kuishirikisha sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika kuharakisha utekelezaji wa Dira 2050 ili kujenga uchumi jumuishi, shindani na unaotegemea uzalishaji wenye tija.

**Pili:** Wakuu wa Mikoa simamieni kikamilifu maandalizi na mapokezi ya wanafunzi wa elimumsingi ya lazima ya miaka kumi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2028 kwa kukamilisha miundombinu na huduma zote muhimu.

**Tatu:** Kuimarisha usimamizi wa makusanyo ya mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na mashine za POS, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kuendeleza rasilimali fedha katika miradi ya kimkakati na kielelezo.

**Nne:** Wizara, Taasisi na Mamlaka zinazoshiriki katika uwezeshaji wananchi kiuchumi ziweke malengo yanayopimika, viashiria vya utendaji na ratiba za utekelezaji, ili kuhakikisha mitaji hiyo inazalisha ajira, kipato na biashara endelevu hasa kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu.

**Tano:** Makandarasi wote wanaotekeleza miradi ya Serikali watimize wajibu wao kwa mujibu wa mikataba waliyoingia ikiwa ni pamoja na kuwalipa watoa huduma walioshiriki kwenye utekelezaji wa mradi husika. Aidha maafisa masuuli kuhakikisha wazabuni na watoa huduma wanalipwa kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano na huduma iliyotolewa.

**Sita:** Wakuu wa Mikoa, ndani ya miezi sita baada ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027 wahakikishe shule zote katika halmashauri zina matundu ya

vyoo kwa kuzingatia uwiano wa wanafunzi waliopo.

**Saba:** Wizara ya Maji ihakikishe huduma ya maji inapatikana kwenye shule na vituo vyote vya kutolea huduma ya afya ndani ya miezi sita baada ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027. Baada ya muda huo, ni marufuku kwa wanafunzi kubeba maji na kupeleka shuleni.

**Nane:** Ubora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika sekta mbalimbali nchini uwiane na thamani ya fedha iliyotolewa. Aidha, fedha zinazoelekezwa na Serikali kwenye miradi hiyo zitumike kama ilivyokusudiwa. Vilevile, makandarasi wa ndani wawe wazalendo kwa kutumia ipasavyo fursa inayotolewa ya ushiriki wa kampuni zilizosajiliwa ndani kutekeleza miradi mikubwa.

**Tisa:** Wizara za Kisekta, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinalipa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali kabla ya kutwaliwa kwa maeneo yao kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

**Kumi:** Taasisi zote za umma kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali ikiwemo mipango, programu na miradi ili kuongeza tija ya utendaji kazi na kuboresha huduma kwa wananchi.

**Kumi na moja:** Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi, Wakala na Idara zinazojitegemea kuanza kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kutathmini Maboresho ya Mfumo wa Kodi kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais.

## SALAMU ZA PONGEZI

*282.* ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa *Balozi Dkt.* Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu. Ninamtakia afya njema na nguvu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza vema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hakika uongozi wake thabiti na mapinduzi makubwa ya kiuchumi anayoyafanya yanaonesha nia ya dhati ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 kwa vitendo.

284. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza na kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Musa Azzan Zungu, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge letu. Ninawaombea heri na baraka za Mungu katika kuongoza mijadala yote ya Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la 13. Sote tuungane kuombea mafanikio mkutano huu na kumwombea Mheshimiwa Spika na wasaidizi wake hekima katika kusimamia shughuli zote za Bunge kama zilivyopangwa.

285. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza pia, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa *Dkt.* Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa *Dkt.* Johannes Lembulung Lukumay, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya

Jamii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu, Mbunge wa Viti Maalum; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Jimbo la Missenyi. Maoni na ushauri wa Kamati hizo yamesaidia sana kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2026/2027.

286. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo wakati wote imekuwa ikisaidia kuboresha mipango na shughuli zinazotekelezwa na Serikali katika kuwahudumia wananchi. Ninaamini mijadala katika Mkutano huu itaendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu.

287. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 07 Machi, 2026, Mheshimiwa Balozi Stephen Patrick Mbundi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kabla ya uteuzi huo, Mheshimiwa Balozi Mbundi alikuwa Katibu

Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayesimamia masuala ya Afrika Mashariki. Kipekee ninampongeza Balozi Mbundi kwa uteuzi huo na kumtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake mapya.

288. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninatoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na wawakilishi wa nchi yetu katika taasisi za kikanda na kimataifa ikiwemo Bunge la Afrika, Jukwaa la Kibunge la SADC, Umoja wa Mabunge Duniani na Jukwaa la Kibunge la nchi zinazozunguka Ukanda wa Maziwa Makuu. Ninawatakia kila la heri katika kuwakilisha na kutetea maslahi ya nchi katika taasisi hizo na kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa.

289. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa *Dkt.* Lazaro Bunungu Komba, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Peramiho kuwa mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi wa Peramiho wamekuamini pasina shaka kuwa utawawakilisha vema. Aidha, ninakukaribisha Bungeni na kukutakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yako ya kuwakilisha wananchi.

290. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Mashirika, Wakala na Idara Zinazojitegemea kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Hakika utendaji wao unaleta tija kubwa sana katika kutekeleza majukumu ya Serikali.

291. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mheshimiwa Hamza Saidi Johari Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushauri wake wakati wote. Vilevile, ninamshukuru sana Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, kwa ushirikiano wake wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, kipekee ninamshukuru ndugu Baraka Ildefophonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa uratibu wa shughuli za kila siku za Bunge na ushirikiano anaoutoa kwa Waheshimiwa Wabunge.

292. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na watendaji wote wa Mahakama kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia na kuimarisha mifumo ya utoaji wa haki. Jitihada zao zimekuwa chachu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuhakikisha haki inapatikana kwa Watanzania wote.

293. ***Mheshimiwa Spika***, kwa moyo wa dhati, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wakuu wa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kulinda Taifa letu. Vilevile, niwapongeze maafisa na askari wote wa majeshi yetu kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kudumisha amani ya nchi yetu. Wakati wote wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa ubunifu, uzalendo, utii, ujasiri na weledi. Hakika tunatambua, tunathamini na tunawashukuru sana kwa moyo wa kizalendo na uwajibikaji wao.

294. ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru viongozi na watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaomba niwataje wachache kwa niaba ya wengi waliofanya wepesi katika utendaji wangu wa kazi za kila siku. Ninamshukuru Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe, Mbunge wa Lushoto na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

295. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, niwashukuru Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na

Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Rahma Riyadh Kisuo, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano); Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI-Elimu); na Mheshimiwa *Dkt*. Jafar Rajab Seif, Mbunge wa Busanda na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI - Afya) kwa kuendelea kunishauri vema na kunisaidia kutekeleza majukumu ya Serikali.

296. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninawashukuru Makatibu Wakuu *Dkt*. Jim James Yonazi (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Bi. Mary Ngelela Maganga (Kazi, Ajira na Mahusiano), Bw. Adolf Hyasinth Ndunguru (TAMISEMI); Naibu Makatibu Wakuu Dkt. James Henry Kilabuko (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Bi. Zuhura Yunus Abdallah (Kazi, Ajira na Mahusiano), *Mhandisi* Rogatius Hussein Mativila (TAMISEMI - Miundombinu), Bw. Sospeter Mambile Mtwale (TAMISEMI), Bw. Atupele Webster Mwambene (TAMISEMI - Elimu), Prof. Tumaini Joseph Nagu (TAMISEMI - Afya); Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

297. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawashukuru watumishi wote wa umma na sekta binafsi kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa. Nikiri kwamba michango yenu ni mikubwa katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wenye tija wa shughuli za Serikali kwa mujibu wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2025/2026.

298. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kitaifa, kikanda na kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga uchumi na kuiletea nchi yetu maendeleo. Michango yao imekuwa muhimu katika kuwezesha nchi yetu kupiga hatua kimaendeleo kwa kuzingatia mipango tuliyojiwekea.

299. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Sekta Binafsi kwa kuendelea kuwa mshirika mkuu wa Serikali katika kuiletea nchi yetu maendeleo. Ushiriki wao umekuwa chachu ya kuchochea ukuaji wa uchumi na kuzalisha fursa za ajira kwa Watanzania. Niwahakikishie wadau wote, Serikali itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kufikia malengo ya Dira 2050.

300. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kushirikiana nami na kuniunga mkono katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu ya Serikali. Hali hii inaonesha ni kwa namna gani wamekuwa wastahimilivu na waungwana kwa Serikali yao katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya pamoja.

301. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Imani na ushirikiano wao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Serikali kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania.

302. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa, ninapenda kumshukuru mke wangu mpendwa Bi. Neema Mwigulu Nchemba, watoto wangu Joshua Mwigulu, Gracious Mwigulu, Isaac Mwigulu, Bernice Mwigulu kwa upendo, uvumilivu na maombi yao. Nikiri kwamba, maombi yao yamekuwa yakinipa nguvu wakati wote ninapotekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa. Ninawashukuru na ninawapenda sana.

303. ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitawashukuru wanahabari ikiwa ni pamoja na waandishi katika mitandao ya kijamii. Nina imani kuwa, mtaendelea kuwahabarisha wananchi kuhusu yanayojiri katika mkutano huu wa Bunge pamoja na masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi na hivyo kuimarisha umoja na mshikamano wa Kitaifa.

## HITIMISHO

304. ***Mheshimiwa Spika,*** nihitimishe hotuba yangu kwa kuwaahidi wananchi kuwa Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kuwatumikia kwa moyo wa dhati kwa kuzingatia kaulimbiu ya ***Kazi na Utu - Tunasonga Mbele***. Katika kuhakikisha hilo, ninasisitiza watumishi wote wa umma kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kutoa huduma bora kwa wananchi bila upendeleo.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2026/2027

### Makusanyo ya Mapato

305. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani ya jumla ya shilingi **2,411,548,152,302.47.**

Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama ilivyo kwenye **Jedwali Na. 1**.

| **Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa Mwaka 2026/2027** | |
|---|---|
| **Jina la Ofisi** | **Makusanyo (Shilingi)** |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu | 12,020,000,000.00 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 2,336,528,152,302.47 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano | 63,000,000,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **2,411,548,152,302.47** |

## Matumizi

306. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2026/ 2027, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 12,502,356,160,000.00** kati ya fedha hizo, **shilingi 8,734,043,089,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 3,768,313,071,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

307. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 225,021,780,000** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **shilingi 207,992,798,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 17,028,982,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha za matumizi ni kama ilivyo kwenye

**Jedwali Na. 2**.

| **Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2026/2027** | |
|---|---|
| **Jina la Ofisi** | **Makusanyo (Shilingi)** |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu | 183,950,342,000.00 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 12,268,472,643,000.00 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano | 49,933,175,000.00 |
| **JUMLA** | **12,502,356,160,000** |
| **Mfuko wa Bunge** | **225,021,780,000.00** |

308. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja.